# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**FEBRUARI, 2024**

YALIYOMO UKURASA


SEHEMU YA KWANZA.......................................................................................... 01

1.0 UTANGULIZI……………………………………………………………………. 01

1.1 MUUNDO WA KAMATI…………………………………………………….... 02

1.2 UTARATIBU WA KAZI ………………………………………………………. 03

SEHEMU YA PILI ……………………………………………………………….. 04

2.1 USANYAJI WA MAPATO…………………………………………………… . 05

2.3 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR …….. 06

2.8 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) ………………. 09

SEHEMU YA TATU ……………………………………………………………..… 12

3.1 WIZARRA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI…………………..……… 12

3.5 USARIFU NA UWANIKAJI DAGAA……………………………………..… 14

3.8 UJENZI WA BOTI ZA UVUVI ……………………………………………….. 17

3.1.2 UGAWAJI WA BOTI ZA UVUVI NA BOTI ZA MWANI………………… 18

SEHEMU YA NNE……………………………………………………………….… 22

4.0 WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI MALIASILI NA MIFUGO…………. 22

4.5 MIRADI YA UMWAGILIAJI………………………………………………….. 23

4.1.1 KITUO CHA UTAFITI WA MIFUGO (CHANANGWE- PEMBA) ……… 27

4.1.3 KITUO CHA MIFUNGO DONGE MUWANDA ………………………… 29

4.1.6 MISITU YA HIFADHI …………………………………………………….. 31

4.1.9 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA

NA ZANA ZA KILIMO …………………………………………………………. 34

4.2.3 IDARA YA UMWAGILIAJI ……………………………………………… 36

4.2.6 AFISI YA AFIASA MDHAMINI ………………………………………………….. 37

4.2.9 MACHINJIO YA WANAYAMA ……………………………………………... 38

SEHEMU YA TANO ……………………………………………………………… 41

5.1 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA…………………... 41

5.4 UKUSANYAJI WA MAPATO…………………………………………………… 42

5.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) …………………………………… 43

5.8 TAASISI YA WIWANGO ZANZIBAR (ZBS) ………………………………….. 47

5.1.2 TAASISI YA USAJILI WA HAKIMILIKI (CUSOZA) …………………………... 50

5.1.5 KIWANDA CHA MWANI PEMBA……………………………………………... 52

SEHEMU YA SITA ……………………………………………………………………... 54

6.0 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE…………………………………… 54

6.2 MRADI WA KUIMARISHA ENEO LA KIHISTORIA LA

RAS MKUMBUU PEMBA………………………………………………………….. 55

6.5 MRADI WA KUIMARISHA ENEO LA KIHISTORIA LA MANGAPWANI

UNGUJA ……………………………………………………………………………... 56

6.8 KAMISHENI YA UTALII…………………………………………………………… 58

6.1.2 HITIMISHO……………………………………………………………………….. 61

# RIPOTI YA KAMATI YA UTALII, BIASHARA NA KILIMO

# YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024.

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu Kanuni ya 107, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020. Kamati hiyo imepangiwa kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na ya Wananchi ya Wizara husika;
iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
v. Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika;

Katika kutekeleza majukumu yaliyopo hapo juu, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo inasimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara tano zifuatazo:

- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi
- Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda
- Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na
- Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

## 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi imeundwa na Wajumbe wanane wafuatao:

1. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Mwenyekiti
2. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Mjumbe
4. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Mjumbe
5. Mhe. Said Saleh Salim - Mjumbe
6. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa- Mjumbe
7. Mhe. Suleiman Makame Ali - Mjumbe
8. Mhe. Dr. Mohamed Ali Suleiman - Mjumbe

Aidha, Kamati ina makatibu watatu na msaidizi mmoja ambao ni:

1. Ndg. Yussuf Mkamba Mwinyi - Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu
3. Ndg. Abubakar Mahmoud Idd - Katibu
4. Ndg. Azmina Khamis Hamad - Msaidizi

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI

Katika utekelezaji wa majukumu yake yaliyoainishwa na Jadweli la Kwanza la Kanuni ya 107 ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, Kamati ilifanya kazi kwa utaratibu wa kupokea taarifa tofauti za kila robo mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa maoni, maagizo na ushauri wa kutatua changamoto hizo.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilifanya kazi kwa mizunguko mitatu (3) kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

1. Mzunguko wa kwanza ulianzia tarehe 14 hadi tarehe 18 Agosti 2023 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 21 hadi tarehe 25 Agosti 2023 kwa upande wa Unguja.
2. Mzunguko wa pili ulianzia tarehe 06 Novemba hadi tarehe 10 Novemba 2023 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 13 Novemba hadi tarehe 17 Novemba 2023 kwa upande wa Tanzania Bara.
3. Mzunguko wa tatu ulianzia tarehe 15 Januari hadi tarehe 26 Januari 2024, Unguja.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina jumla ya Wafanyakazi 395 ( kati ya hao 311 wako Unguja na 84 wako Pemba) inayojumuisha Wanawake 205 na Wanaume 190. Aidha,Ofisi imeundwa kwa Idara saba, Taasisi mbili zinazojitegemea pamoja na Bodi zake na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

Idara hizo ni pamoja na: -

1. Kamisheni ya Kazi;
2. Ajira;
3. Usalama na Afya Kazini;
4. Maendeleo ya Vyama vya Ushirika;
5. Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
6. Uendeshaji na Utumishi;
7. Mipango, Sera na Utafiti na
8. Ofisi Kuu Pemba.

Ofisi ina Taasisi zifuatazo: -

1. Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na
2. Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA).

Bodi za Usimamizi za Taasisi ni pamoja na:-

1. Bodi ya Wakurugenzi yaMamlaka ya Kukuza Uwekezaji;
2. Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
3. Bodi ya Mishahara na
4. Bodi ya Ushauri wa Kazi.

## 2.1 UKUSANYAJI WA MAPATO

### Fungu A07

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ilitarajiwa kukusanya Mapato ya jumla ya TSh.1,456,867,076 hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2023, Afisi imefanikiwa kukusanya mapato ya TSh.2,434,247,764 sawa na asilimia 167% ya lengo kupitia vianzio vyake 4, ikiwemo ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi.

Kwa upande wa matumizi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A07 kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023-2024, ilikadiriwa matumizi ya jumla ya TSh. 3,825,702,494. Kati ya fedha hizo, TSh. 2,138,068,789 ni kwa ajili ya Mishahara; na TSh.1,687,633,705. ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023-2024, fedha zilizoingizwa kwa matumizi kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) ni TSh. 2,964,835,808 sawa na asilimia 77 ya makadirio. Kati ya fedha hizo, TSh. 2,138,068,789 za mishahara sawa na asilimia 100 ya makadirio na TSh. 826,767,019 sawa na asilimia 49 ya makadirio kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha zilizoingizwa kwa miradi ya Maendeleo.

### Fungu A08

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Kipindi cha Julai – Disemba, 2023-2024 kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji) ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh. 8,274,307,787 Kati ya fedha hizo, Tsh. 2,110,925,547 ni kwa ajili ya Mishahara, na Tsh. 567,556,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tsh. 5,595,826,240 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023, fedha zilizoingizwa kwa matumizi ni Tsh. 6,264,675,608 sawa na asilimia 75.7 ya utekelezaji wa Programu zote kwa kipindi hicho. Kati ya hizo Tsh.2,171,999,368 zilitumika kwa Mishahara ambayo sawa na asilimia 102.9 ya makadirio. Aidha, Tsh. 246,850,000) ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo sawa na asilimia 43.5 ya makadirio. Na Tsh.3,845,826,240.00 sawa na asilimia 68.7 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

## 2.2 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zilizobainika, Kamati inaagiza yafuatayo:

1. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara kibali cha uajiri kwa nafasi zinazohitaji wataalamu wa fani maalum ambazo zitarahisisha utendaji wa Kamisheni ya Kazi.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kujitahidi katika kutoa fedha za matumizi mengineyo kwa wakati na kwa mujibu wa (Cash Flow) ili shughuli za Wizara ziweze kutekelezwa kwa mujibu wa mipango waliyojipangia.

3. Kamati inaishauri Wizara kufikiria namna ya utanuzi wa ofisi yake kwa kuanza kutafuta wafadhili au kuomba fedha Serikalini kwa ajili kujenga jengo la kisasa ambalo litakuwa na nafasi ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya Idara zake zote.

4. Kamati inaiagiza Wizara kutenga fedha maalum kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi kama vile samani na kompyuta kwa kila Idara.

## 2.3 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR (ZEEA)

Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (Zanzibar Economic Empowerment Agency - ZEEA) imeanzishwa kwa Sheria namba 2 ya mwaka 2022 kwa lengo la kuimarisha mazingira wezeshi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuongeza tija, uzalishaji, ufanisi na masoko ya bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara nchini. Taasisi hii imeundwa kwa kuziunganisha Idara mbili zilizokuwepo awali; Idara ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Wananchi Kiuchumi; na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

## 2.4 MAJUKUMU YA (ZEEA)

Kwa mujibu wa kifungu namba 6 cha sheria namba 2 ya mwaka 2022, majukumu ya ZEEA ni:-

1. Kutoa ushauri kwa Serikali, Taasisi za umma na binafsi kwa mambo mahsusi na njia zinazolenga katika kushajihisha uwezeshaji kiuchumi Zanzibar;
2. Kuratibu programu za mafunzo na elimu, huduma za ushauri elekezi, masoko na utoaji wa mitaji kwa mjasiriamali au mfanyabiashara;

3. Kuwatambua, kuwahakiki na kuwaunganisha Wajasiriamali au Wafanyabiashara na Taasisi za Kifedha.
4. Kuanzisha na kuendeleza mfumo wa usimamizi wa taarifa wa shughuli za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi katika sekta mbali mbali na na kuwezesha usambazaji wa taarifa;
5. Kupendekeza juu ya namna na njia za kuchukua zitakazohakikisha upatikanaji wa huduma za mikopo;
6. Kuchunguza au kukagua nyaraka zinazohusiana na mwenendo wa mjasiriamali au mfanyabiashara;
7. Kumtambua mjasiriamali au mfanyabiashara mwenye sifa kwa madhumuni ya kumuingiza katika programu za uwezeshaji;
8. Kutambua na kufanya utafiti wa masoko ya bidhaa na huduma zinazotolewa na mjasiriamali au mfanyabiashara;
9. Kuwezesha utoaji wa mkopo na kuhakikisha unarudishwa kwa wakati;
10. Kumuunganisha mjasiriamali au mfanyabiashara na vituo vya mafunzo vya amali n.k

## 2.5 MAFANIKIO

Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, ZEEA ilipata mafanikio yafuatayo:-

1. Imeunda kamati 11 za Mamlaka za Serikali za Mitaa zikiwa na lengo la kuratibu Mfuko wa Makundi Maalum ya Wajasiamali (4:4:2) unaotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
2. Imeunda kamati ya kuthibitisha maombi ya mikopo kwa Programu ya Khalifa na Kamati ya Zabuni ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar.
3. Imeandaa Mfumo wa Utoaji wa Mikopo kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao.
4. Imesaini Makubaliano ya ushirikiano na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuwawezesha wananchi.

### 2.6 CHANGAMOTO

Mbali na mafanikio yaliyopatikana, Wakala inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Uhaba wa rasilimali watu.
2. Kutokuwa na jengo la Ofisi.
3. Uchelewaji wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa mujibu wa 'Cash Flow' ambao unapelekea kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya kazi.
4. Kutokuwepo kwa Sheria na Kanuni ya kuwashtaki wadaiwa sugu wa Mfuko wa Uwezeshaji.
5. Serikali za mitaa kutochangia kikamilifu asilimia kumi ya mapato yatokanayo na makusanyo ya ndani kama ilivyoelekezwa kwa mujibu wa Sheria.
6. Wananchi wengi kutokuwa na elimu ya uanzishaji wa miradi kwa ajili ya kupatiwa mikopo ya uwezeshaji na hatimae kutoa malalamiko kwa viongozi wao wakati wanapokataliwa maombi yao.

### 2.7 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zinazoikabili ZEEA, Kamati inaagiza mambo yafuatayo:

1. Tayari Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar imewasilisha mahitaji ya wafanyakazi katika Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma (ORKSUU) na kuelekezwa kusubiri utaratibu wa kuunganisha taasisi ukamilike kabla ya kutolewa kibali cha ajira mpya, hivyo Kamati inashauri baada tu ya taratibu hizo kukamilika wakala ipewe kibali cha uajiri kwa haraka ili iweze kufanya kazi zake kwa weledi mkubwa.

2. Kamati inaiagiza Serikali iharakishe mchakato wa kupatiwa ofisi wakala kwa vile tayari Serikali imekubali kutatua changamoto hiyo.
3. Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kwa mujibu wa "Cash flow' Kwa lengo la kutekeleza ipasavyo shughuli za wakala kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa.

4. Kamati inaiagiza Wizara kupitia Wakala kuharakisha mchakato wa kutayarisha Kanuni ya Sheria nambari 2 ya mwaka 2022 ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo kuthibiti upotevu wa fedha za mikopo kwa wananchi ambao hawarudishi mikopo hiyo kama walivyokubaliana katika mkataba husika.

5. Kamati inaagiza Wizara kuwasiliana na Wizara inayosimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Sheria kwa kuchangia asilimia 10 ya mapato ya ndani kwenda katika Wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kusaidia makundi maalum ya vijana, watu walemavu na wajasiriamali.

6. Kamati inishauri Wakala iendelee kutoa elimu Zaidi juu ya uanzishaji wa miradi yenye tija kwa wananchi na inayoweza kupatiwa mikopo ili kila mwanachi aweze kunufaika kupitia mfuko huu wa uwezeshaji na hatimae marejesho ya mkopo yaweze kupatikana ipasavyo.

## 2.8 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar ni Taasisi ya Serikali inayofanya kazi chini ya Sheria ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2023. Jukumu la msingi la Mamlaka hii ni kutekeleza sera na Sheria ya Uwekezaji kikamilifu kwa nia ya kuwavutia wawekezaji wenye tija kwa manufaa ya nchi na wananchi wake.

Serikali, kupitia Mamlaka hii imeelekeza nguvu zake katika kutangaza na kusimamia Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2008 katika sekta zote zinazohusika. Aidha, mkazo maalum umewekwa kwenye uimarishaji wa uchumi wa buluu ikizingatiwa kuwa jiografia ya Zanzibar ni visiwa na ina uwanja mpana wa kuimarisha sekta hiyo.

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar ilipewa agizo la kutangaza fursa za uwekezaji katika baadhi ya visiwa hivyo ili kupata wawekezaji makini watakaowekeza uwekezaji wenye tija kubwa kwa nchi na wananchi kwa ujumla. Hivyo, Serikali kupitia ZIPA iliandaa tangazo la ukodishwaji wa visiwa hivyo na ilitayarisha vipengele ikiwa ni muongozo wa kufanya maombi ya uwekezaji katika visiwa hivyo. Aidha, vipengele hivyo vilitumika katika kufanya tathmini ya maombi ya visiwa kwa wawekezaji walioonesha nia ya kutaka kuwekeza katika visiwa hivyo. Katika vigezo vya msingi vilivyozingatiwa kumpata muwekezaji ni ushindani wa bei/mahari (Lease Acquistion Cost-LAC), mtaji utakaowekezwa na wazo la biashara (business concept).

Katika awamu ya kwanza ya kuvitangaza visiwa hivyo, jumla ya visiwa 10 vilitangazwa na awamu ya pili visiwa tisa (9) vilitangazwa.Baadhi ya Visiwa vilivyotangazwa vilipata wawekezaji na

baadhi havikupata. Aidha, baadhi ya visiwa vilitolewa kwa Wawekezaji kupitia Serikali kuu, ambavyo havikuwemo katika visiwa vilivyotangazwa awali.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, visiwa 15 vimekodishwa ambavyo vitajengwa hoteli za kisasa zenye kuzingatia Uhifadhai wa Mazingira na Rasilimali ya Bahari. Jumla ya Dola za Kimarekani Milioni ishirini na Sita (USD 26,000,000) zilikusanywa kama LAC kupitia visiwa vilivyokodishwa na vinatarajiwa kuwekeza jumla ya Dola za Kimarekani milioni mia tatu themanini na nne nukta nne (USD 384.4 milioni). Visiwa vyote hivyo vimekodishwa kwa mujibu wa taratibu na Sheria ya Ardhi zinavyoelekeza ambapo kila mwekezaji amepatiwa miaka thelathini na tatu (33) na itaongezwa hadi kufikia tisini na tisa wakati muwekezaji atakapoomba kuongezewa.

Uwekezaji katika visiwa vidogo vidogo unatarajiwa kuleta faida zifuatazo;

i. Kuongeza pato la Taifa na kuchangia katika kukuza Uchumi wa Nchi;
ii. Kuwa na uwekezaji wa hadhi ya juu unaozingatia utunzaji wa mazingira yaliyopo;
iii. Kuvutia uwekezaji na utalii wa mitaji mikubwa kwenye visiwa vidogo vidogo kama vile inavyofanyika katika nchi za Maldives na Singapore;
iv. Kuimarisha ustawi na maendeleo ya jamii zilizo katika visiwa hivyo;
v. Kuzidisha haiba na thamani ya visiwa vidogo vidogo na mazingira yanayovizunguka; na
vi. Kuongezeka kwa fursa za ajira hasa kwa vijana, wanawake na jamii kwa ujumla.

## 2.9 CHANGAMOTO.

Mbali ya mafanikio yaliyopatikana, ZIPA inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Wakati wa ujenzi ndani ya visiwa hivyo, kumejitokeza hali ya kulazimika kuwepo kwa uharibifu wa Mazingira ambapo wawekezaji hutakiwa kurejesha mazingira hayo kwa kupanda miti ili kuhuwisha mazingira hayo.

2. Kukosekana kwa nishati ya umeme katika maeneo ya visiwa vinavyowekezwa ambapo Serikali imeruhusu na inashajihisha kutumika kwa nishati mbadala kama vile nishati ya jua.

3. Baadhi ya uwekezaji huchukua muda mrefu kabla ya kuanza ujenzi.

### 2.1.1 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zilizojitokeza kwa Mamlaka ya Uwekezaji, Kamati inashauri yafuatayo:

1. Licha ya hatua nzuri ya uwekezaji katika visiwa ambayo itasaidia kutoa ajira kwa vijana wetu na kuongeza mapato kwa Serikali lakini suala utunzaji wa mazingira liwekwe kipaombele, hivyo Kamati inaagiza Mamlaka kusimamia vyema suala la urudishaji wa mazingira na uoto wa asili ambao umeathiriwa kutokana na ujenzi unaoendelea katika visiwa hivyo.

2. Kamati inaungana na wazo la Serikali katika kushajihisha matumizi mbadala ya nishati ya jua kwa ajili kuzalisha umeme utakaotumika katika visiwa hivyo ili kupunguza gharama kubwa ya kusambaza umeme wa kawaida kufika katika maeneo hayo yaliyowekezwa.

3. Kamati inaagiza Mamlaka kuwafuatilia kwa karibu wawekezaji ambao wamechukua muda mrefu bila kuanza kuekeza katika visiwa hivyo kwa kuwachukulia hatua mapema iwezekanavyo ikiwemo kuwafutia vibali vyao.

## SEHEMU YA TATU

## 3.1 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### UTANGULIZI

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Idara sita na taasisi nne zinazojitegemea kama ifuatavyo:

IDARA

1. Uendeshaji na Utumishi
2. Mipango, Sera na Utafiti
3. Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Ukijumuisha Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi)
4. Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini
5. Hifadhi za Baharini
6. Afisi ya Afisa Mdhamini – Pemba

TAASISI

1. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari;
2. Kampuni ya Uvuvi;
3. Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Company);
4. Mamlaka ya Kudhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Authority)

## 3.2 UZALISHAJI WA MATANGO BAHARI

Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar imelenga kuboresha maisha ya wananchi kupitia sera ya Uchumi wa buluu na uvuvi, hivyo wanajamii wanatakiwa kushiriki katika shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwemo matumizi endelevu ya rasilimali za bahari kama vile ufugaji wa matango bahari.

Kwa nia ya kuunga mkono juhudi za Serikali ya mapinduzi Zanzibar kupitia sera ya Uchumi buluu na uvuvi, Taasisi ya Marine and Coastal Community Conservation (MCCC) imejenga kituo cha

kutotolesha na uleaji wa vifaranga vya matango bahari katika kijiji cha Kibaridi Pujini Pemba pamoja na kituo cha uzalishaji wa samaki na matango bahari Beital Ras kwa upande wa Unguja. Vituo hivi vilijengwa kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa vifaranga vyenye ubora kwa ajili ya ufugaji endelevu wa samaki na matango bahari.

Lengo kuu la miradi hii ni kuzalisha vifaranga vya matango bahari ili kuwawezesha wafugaji wa matango bahari wa Zanzibar kupata vifaranga vya matango bahari wakati wote kwa ajili ya kuwa na uzalishaji endelevu wa matango bahari.

Maeneo ya miradi hii lilichaguliwa kwa vigezo maalum vikiwemo utayari wa wanajamii, upatikanaji wa maji safi ya baharini, chanzo cha maji baridi, upatikananji wa miundombinu ya barabara pamoja na huduma ya umeme ambapo maeneo ya Pujini Beit al Ras yaliteuliwa kuanzishwa vituo hivyo. Uchaguzi wa maeneo ya ujenzi wa vituo hivyo ulifuatiwa na ulipaji wa fidia ya vipando vilivyokuwepo katika maeneo hayo.

## 3.3 CHANGAMOTO

Pamoja na maendeleo mazuri ya miradi hii, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

1. Mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaathiri uzalishaji wa chakula kwa ajili ya vifaranga
2. Ukosefu wa taaluma bora na ya kisasa zaidi juu ya uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari
3. Kwa upande wa Beit al Ras, Upatikani wa maji ya chumvi kwa ajili ya kulea vifaranga kwa njia ya kuchota maji baharini ni njia ambayo inapoteza muda na sio salama kwa afya ya utoleshaji na ukuzaji wa vifaranga katika (Hatchetry).
4. Wananchi na wafugaji kutokuwa na uelewa wa kutosha wa jinsi ya upatikanaji na ufugaji wa kitaalamu wa vifaranga hivyo, kwani wananchi wanapopatiwa vifaranga hivyo kwa ajili ya ufugaji katika mabwawa yao huwa havifikii malengo katika ukuaji wake na hatimae kufariki na tija iliyokusudiwa kushindwa kupatikana.

### 3.4 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, Kamati inaagiza yafuatayo:

1. Kamati inashauri kuanzishwa kwa vituo vyengine vya uzalishaji wa vifaranga vya matango bahari nchini ili kuimarisha ufugaji wa viumbe hivyo na kupunguza kasi ya uvunaji kutoka baharini.
2. Kamati inaagiza Serikali kuwaendeleza vijana wanaokiendesha kituo hiki ili kuwa wabobezi kwenye fani zao kwa maendeleo ya uchumi wa buluu nchini.
3. Licha ya Kamati kuelezwa kuwa kituo cha kutotoleshea vifaranga kinafanya utaratibu wa kuunganisha bomba hadi baharini kwa ajili kupata maji ya chumvi, Kamati inapendekeza kufanya utafiti ili kubaini ni kina gani cha maji kitafaa kwa ajili ya kuvutwa kulingana na aina ya vifaranga hivyo ili kuepusha kuathiriwa ukuaji wake na kukosa sifa katika masoko mbalimbali ambayo tunatarajia kuuza bidhaa hizo.
4. Aidha Kamati inashauri Wizara kupitia kituo hicho kuyatembelea mabwawa ya wananchi wanaofuga vifaranga hivyo na kuendelea kutoa elimu mbalimbali juu ya namna ya kuendeleza ufungaji wa vifaranga kitaalamu kwa lengo la kuendeleza ufugaji huo na bidhaa inayopatikana iweze kuwa na sifa na viwango stahiki na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana.

### 3.5 USARIFU NA UANIKAJI DAGAA

Uvuvi wa dagaa ni shughuli ya kiuchumi inayofanywa na wananchi wengi wa maeneo ya ukanda wa bahari. Zanzibar ni sehemu maarufu kwa uzalishaji wa dagaa ambalo hutumika kwa kitoweo katika soko la ndani na nje ya nchi. Soko kuu la dagaa wa Zanzibar ni Kongo na Tanzania Bara. Kwa kutambua fursa iliyopo kwenye biashara hii, Serikali kupitia Kampuni ya Uvuvi ZAFICO imeamua kuirasimisha na kuiongezea thamani ili ilete tija kubwa kwa wafanya biashara wenyewe na Taifa kwa ujumla ambapo miradi miwili imeanzishwa kwa ajili ya kusarifu na kuongeza thamani ya dagaa. Miradi hiyo ni Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa - Ndagoni na Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa - Kama.

Kwa kutambua umuhimu wa miradi hii, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeyachagua maeneo ya Ndagoni na Kama kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kusarifu dagaa kwa nia ya kuwasaidia na kuwakomboa wajasiriamali wa dagaa kutoka katika uzalishaji wa kawaida na kwenda katika uzalishaji mkubwa wa kibiashara. Lengo kuu la kuanzishwa kwa mradi huu ni kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa ili wananchi waweze kupata bei nzuri katika soko la ndani na la Kimataifa ili waweze kujikwamua kimaisha na kuongeza kipato.

### 3.6 CHANGAMOTO

Licha ya nia njema ya Serikali ya kuanzisha miradi hii, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

1. Wanajasiriamali wanaoendesha shughuli zao katika eneo la Ndagoni wamezowea kukausha dagaa kwa kulianika bila ya kulichemsha jambo ambalo linatofautiana na mpango wa kiwanda hicho ambacho kitaweka miundombinu ya kuchemshia kwa njia ya kisasa.

2. Uanikaji wa dagaa hufanyika kwa njia za kiasili (kuanikwa chini) na kuifanya bidhaa hiyo kushuka thamani kutokana na kuchanganyika na mchanga.

3. Wasajisiriamali wa dagaa hawana miundombinu ya kuhifadhia bidhaa yao na pindi mvua inaponyesha dagaa lote huharibika.

4. Miundombinu isiyo rafiki na uchimbaji wa mchanga unaopelekea ugumu wa kulifikia eneo la Ndagoni pamoja na kuwepo kwa mashimo yenye maji maeno hayo.

5. Kutokamilika kwa wakati ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa kilichopo kama, ambapo ilitarajiwa kwa lot namba 1 Mradi huo uwe umekamilika kwa asilimia 100 ifikapo Disemba 2023, wakati Kamati ilipotembelea Mradi huo tarehe 19/01/2024 imeelezwa kuwa ujenzi wa Lot 1 umefikia asilimia 70 ambapo sehemu iliyobaki ni ujenzi wa land scape ambao

imechelewa kutokana na kunyesha kwa mvua za mara kwa mara hali inayopelekea vifaa vya ujenzi kama vile Doza kukwama kutokana mazingira yaliyopo katika eneo la mradi.

6. Kuwepo kwa Mkandarasi msaidizi (sub contract) ambae hana uwezo na ameshidwa kumaliza kazi zake kwa wakati na hatimae Mkandarasi huyo kuondoshwa kwa agizo la Mheshimiwa Rais.

7. Ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathiriwa na Mradi, Kamati imeelezwa kuwa wananchi ambao waliokua wakifanya shughuli zao za kijamii katika maeneo hayo watalipwa fidia zao lakini cha kushangaza hadi Kamati inaondoka katika eneo hilo fidia hizo bado hazijalipwa.

### 3.7 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiagiza Wizara kuharakisha ujenzi wa kiwanda hiki ili kuwapa fursa wajasiriamali wa dagaa nchini kufanya shughuli zao kwa njia za kisasa na kupata faida nzuri.
2. Pamoja na kuwa nae neo la ujenzi ambalo limeshapimwa , Kamati inaishauri Wizara kuangalia uwezekano wa kuongeza eneo hilo ili liwe kubwa zaidi na kuliombea hati.Ili kutoa fursa ya utanuzi wa kiwanda hichi pale hati itakaporuhusu.
3. Kamati inaiagiza Wizara kulifuatilia kwa karibu suala la upatikanaji wa fidia za wananchi wanaokua wakilitumia eneo hilo kwa shughuli mbalimbali na kupatikana fidia hizo kabla ya kuanza ujenzi wa kiwanda hiki.
4. Kamati inaishauri Wizara kuwaelimisha wanajamii juu ya umuhimu wa kiwanda hicho kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla ili wanajamii hao waweze kutoa ushirikiano wa kutosha katika kukilinda kiwanda hicho.
5. Kamati inaiagiza Wizara kupitia Kampuni ya ZAFICO kusimamia vizuri ujenzi wa Mradi wa Kiwanda cha kusarifu dagaa - Kama kwa (phase) zote mbili ili kuweza kukamilika kwa wakati na tija iweze kupatika kwa wananchi.
6. Kamati inaishauri Wizara kuwa makini katika kutafuta wakandarasi wenye sifa na weledi wa kazi mbalimbali za ujenzi ili kuepusha kutokamilika kwa wakati miradi inayotekelezwa na Wizara na hatimae kuingizia hasara Serikali.

7. Kamati inaiagiza Wizara kuchukua hatua za haraka kuharakisha mchakato wa ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao wameathiriwa na Miradi hiyo kwa maeneo yote mawili (Kama na Ndagoni) ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima baina ya wananchi na Serikali yao na hatimae Miradi hiyo iweze kutekelezwa bila ya malalamiko yoyote kutoka kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

### 3.8 UJENZI WA BOTI ZA UVUVI

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeingia mikataba na Kampuni mbali mbali kwa ajili ya utengenezaji wa boti za uvuvi zenye ukubwa wa mita 5, 7 na 8, ikiwa ni hatua moja ya utekelezaji wa sera ya Uchumi wa buluu kivitendo. Kampuni hizo ni:

- Songoro Marine servises
- DMG
- Qiro group of company
- Dhowlishers
- Captain Andi
- Ocean Enterprises

Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ilitembelea baadhi ya Kampuni hizo na kubaini kasi ndogo ya ujenzi wa boti kutokana na sababu tofauti. Pia, Kamati imebaini kuwa baadhi ya kampuni zilizopewa kazi hazikuwa na uwezo wala sifa ya kufanya kazi hiyo.

### 3.9 CHANGAMOTO

Licha ya malengo mazuri ya Serikali ya kutekeleza mradi huu, ujenzi wa boti bado unakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Kamati imebaini kuwa kampuni zilizopewa kazi ya utengenezaji wa boti hazikuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo na kupelekea kuchelewa kumalizika kwa kazi hiyo.
2. Kamati imepatiwa majibu tofauti kutoka kwa Wizara, Benki ya CRDB na Kampuni za ujenzi wa boti juu ya suala la upatikanaji wa mashine za YAMAHA . Hali hii inadhihirisha kukosekana kwa ushirikiano baina ya wadau hao.

### 3.1.1 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, Kamati inaagiza mambo yafuatayo:

1. Wizara iendelee na kazi ya uhamasishaji wa wananchi ili waitumiye ipasavyo fursa ya miradi iliyopo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi na kuongeza pato la Taifa letu.

2. Kamati inaiagiza Wizara kuwasimamia ipasavyo wakandarasi wote ambao wamewapa kazi ya kutengeneza Boti na kuhakikisha wanazikamilisha kazi zao kwa wakati kwa lengo la kuwapatia wavuvi Boti zao.

3. Kutokana na dhamira ya dhati ya Serikali kuwakomboa wavuvi na kuwafanya wajitegemee wenyewe kwa kuwa na vyombo vyao, Kamati inawashauri wavuvi watakaokabidhiwa vyombo hivyo kuvitunza ili vidumu kwa muda mrefu zaidi na kuleta tija iliyokusudiwa.

4. Kamati inaiagiza Wizara kuhakikisha ubora na uwezo wa kampuni kila inapotaka kuingia mikataba kwa shughuli mbali mbali kabla ya kufunga mikataba na kampuni hizo ili kuepusha kukwama njiani kwa mikataba hiyo.

### 3.1.2 UGAWAJI WA BOTI ZA UVUVI NA BOTI ZA MWANI

Wizara inaendelea na program ya ugawaji wa boti za uvuvi na za mwani ambapo jumla ya TZS Bilioni 36.5zilitengwa kupitia programu ya UVIKO 19 ambapo TZS Bilioni 28.8zilizowekwa Benki ya CRDB kwa ajili ya Programu ya Maboti na Kiwanda cha kusarifu dagaa na TZS Bilioni 7.7kwa matumizi ya uwezeshaji (Ujenzi wa Mabwawa ya samaki, kaa matango bahari na mafunzo). Kati ya fedha zilizowekwa CRDB Bank TZS 28.8 BilioniJumla ya TZS 13.8tayari zimetumika kwa maboti.

### 3.1.3 CHANGAMOTO

Zoezi la ugawaji wa boti linakabiliwa na changamoto zifuatazo:

1. Ucheleweshaji wa upatikanaji wa boti kwa wananchi ni jambo linalorudisha nyuma jitihada za wavuvi katika kujikwamua kuichumi, baadhi ya vikundi vya wavuvi vinafikia muda wa mienzi sita hadi mwaka baada ya kupeleka maombi na wanashidwa kupatiwa boti hizo.

2. Urejeshwaji wa mikopo usioridhisha kwa waliopatiwa mikopo ya boti za aina mbalimbali za uvuvi. Kamati imeelezwa na uongozi wa CRDB kuwa viwango vya urejeshaji wa mikopo haviridhishi na hivyo hupelekea changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya ulipaji wa boti nyengine mpya ambazo zinatarajiwa kukopeshwa kwa wananchi wengine.

3. Kutoshirikishwa kwa Viongozi wa Serikali na Wawakilishi katika utoaji wa boti hizo hali inayopelekea Viongozi mbalimbali kutojua taarifa sahihi za utolewaji wa boti hizo kwa wananchi katika majimbo yao.

### 3.1.4 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zilizojitokeza, Kamati inaagiza yafuatayo:

1. Kamati inaagiza uongozi wa Wizara pamoja na Uongozi wa CRDB Kuhakikisha wanaharakisha mchakato wa kupatiwa boti kwa wananchi au vikundi ambavyo vimekaguliwa na kuonekana vina sifa ya kupatiwa mkopo huo.

2. Aidha Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi juu ya urejeshaji wa mikopo hiyo kwa vile wapo baadhi ya wananchi baada ya kupatiwa mikopo hiyo wanakuwa wagumu kurejesha kwa kisingizo cha kuwa ni fedha ya Serikali na haistahili kurejeshwa na kupelekea kutopatikana mikopo hiyo kwa wananchi wengine ambao wana mahitaji ya mkopo huo.

3. Kamati inaishauri Wizara inapotoa mikopo ni vyema kuwashirikisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka katika majimbo husika ili kuwa na taarifa sahihi ya boti zilizotolewa.

Aidha, ushirikiswaji huo utaweza kusaidia waheshimiwa wajumbe katika kuhimiza na kutoa elimu kwa waliopatiwa mikopo juu ya matumizi mazuri ya boti hizo na urejeshaji wa mikopo hiyo kwa wakati ili na wenzao waweze kunufaika.

### 3.1.5 CHANGAMOTO ZA WIZARA KWA UJUMLA

1. Upungufu wa Watendaji ambapo Kamati imearifiwa kuwa Wizara imewasilisha Serikalini ombo la wafanyakazi wapya na tayari wameanza kuajiri Pemba (35) na Unguja (23).
2. Uhaba wa Teknolojia na nyenzo za kufanyia kazi ambapo Wizara imeomba gari saba ambazo bado hazijapatikana.
3. Kuwepo kwa matukio ya uvuvi haramu
4. Ukosefu wa wataalamu wa uvuvi wa bahari kuu kwa kampuni ya ZAFICO
5. Wizara na jamii kwa ujumla kutorejeshewa sehemu ya mapato yatokanayo na hifadhi ya PECCA ingawa mawasiliano yamefanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

### 3.1.6 MAONI NA MAAGIZO YA KAMATI

Kutokana na changamoto zinazoikabili Wizara, Kamati inaagiza yafuatayo:

1. Kamati inaiagiza Wizara kusimamia kwa karibu zaidi vikundi vilivyoundwa kwa ajili ya ufugaji wa mazao ya baharini na ili kuzijua changamoto zinazowakabili katika shughuli zao na kuzitatua katika hatua za awali ili zisilete hasara kwa wanakikundi.

2. Sambamba na elimu ya ufugaji wa mazao ya baharini wanayopatiwa wanavikundi, Kamati inaagiza wazalishaji wa mazao ya baharini waelimishwe namna ya kufanya ukarabati wa mabwawa ili kukabiliana na upotevu wa maji ambayo ndio msingi kwa uhai wa mazao ya baharini.
3. Ili kuzalisha mazao yenye tija kubwa kwa wakati husika, Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia mwenendo wa soko la dunia katika mazao ya baharini na kuwaelekeza ipasavyo wafugaji wa mazao hayo.

4. Kamati inaiagiza Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango itekeleze kwa vitendo mpango wa mgao wa mapato yanayoingia kwenye maeneo ya hifadhi ya PECCA ili jamii ihamasike zaidi na uhifadhi wa maeneo hayo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaundwa na Idara na Taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi katika kuwaletea maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

### 4 .1 IDARA ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula
4. Idara ya Umwagiliaji
5. Idara ya Misitu
6. Idara ya Maendeleo ya Mifugo
7. Afisi ya Afsa Mdhamini –Pemba

### 4.2 TAASISI ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
2. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo
3. Wakala wa Matrekta na Zana za Kilimo

### 4.3 PROGRAMU KUU ZA WZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inajiendesha kupitia programu kuu tano ambazo ni:

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo;
2. Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;

3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

## 4.5 MIRADI YA UMWAGILIAJI

Kamati ilifanya ziara katika mabonde mbali mbali ya umwagiliaji kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana.

### A. Miradi ya Umwagiliaji maji katika Bonde la Kinyasini (Unguja)

Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika bonde la Kinyasini unakadiriwa kumwagilia hekta 184 za mashamba yote katika bonde hilo. Jumla ya dola Milioni 150 za Kimarekani zimekadiriwa kutumika katika ujenzi wa miundombinu hiyo chini ya Msahuri Elekezi Corea Rural Community. Mradi huu umekamilika kwa asilimia mia moja na takribani wakulima 1,500 wanategemewa kunufaika katika mgao wa mashamba katika eneo hili na hadi Kamati inapokea taarifa hii jumla ya wakulima 1,200 tayari wameshagaiwa maeneo (plots) kwa ajili ya kuanza kulima kwa msimu huu wa kilimo.

## 4.6 CHANGAMOTO ZA MRADI

1. Kukosekana kwa kingo pembezoni mwa madaraja yaliopo katika mradi huu, kunaweza kuhatarisha usalama wa wananchi wanaoishi karibu na wale wanaopita katika maeneo hayo hasa watoto wadogo ambao mara nyingi hupenda kucheza katika sehemu hatarishi.

2. Mradi huu upo karibu na makaazi ya wananchi. Kamati imewabaini baadhi ya Wananchi katika mabonde hayo (Kinyasini) wakivuna maji, hali inayohatarisha usalama wao.

3. Kamati imebaini uingizwaji wa wanyama mabondeni. Wanyama kama vile ng'ombe walionekana katika bonde hali ambayo kwa njia moja au nyengine huharibu miundombinu ambayo imejengwa kwa gharama kubwa na Serikali yetu.

4. Kamati imebaini changamoto kubwa ya upotevu wa maji ambapo kamati ilielezwa kuwa, kwa sasa mradi umekamilika kwa asilimia zote lakini upotevu huo wa maji utasababisha harakati za umwagiliaji katika mashamba ya wakulima kushindikana.

5. Changamoto nyengine iliyowasilishwa mbele ya Kamati ni kukosekana kwa bajeti ya kusaidia utatuzi wa baadhi ya changamoto pale zinapojitokeza.

6. Uharibifu wa mazingira katika kingo za Bwawa la kinyasini kama vile kukata miti pamoja na kuendeleza shughuli za kibinaadamu pembezeni mwa mradi.

7. Mradi kutokua na uzio ni miongoni mwa changamoto ambazo kamati imezibaini katika mradi ambao Serikali imetumia gharama kubwa kuusimamisha.

8. Mradi kua tegemezi, msimu wa kiangazi wakulima hawapati maji kwavile maji hukauka na husabaisha kutokua na mteremko mzuri wa kufika katika mashamba ya wakulima yaliopo bondoni. Hivyo maji yanapatikana kwa wingi katika msimu wa masika tu jambo ambalo litasababisha upungufu wa chakula nchini.

9. Miradi inatumia gharama nyingi kujengwa ila tija yake ni ndogo sana. Fedha zinazotumika haziakisi thamani ya mradi wenyewe na faida haionekani kwa wakulima wanaolima katika maeneo hayo.

### 4.7 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuweka bajeti maalumu ya kusaidia utatuzi wa baadhi ya changamoto pale zinapojitokeza katika utekelezaji wa miradi kama hii.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia Idara ya Kilimo, kuwashirikisha kikamilifu wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayotarajiwa kuanzishwa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kupatiwa ushauri kwani baadhi

ya wakulima wa maeneo hayo wana uzoefu wa kutosha juu ya masuala ya kilimo cha umwagiliaji.

3. Kwa kuzingatia usalama wa wananchi wanaoishi karibu na miundombiunu ya Umwagiliaji maji, Kamati inaishauri Wizara kulichukulia umuhimu wa aina yake suala la kujenga uzio katika maeneo yote ya miradi pamoja na kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo. Aidha, ujenzi huo wa uzio utasaidia sana kuzuia uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi hao.

4. Kamati inaagiza Wizara kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi za Shehia kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la uingizwaji wa wanyama katika mabonde ya Umwagiliaji kwa lengo la kuzuia uharibu wa miundombinu ambayo imejengwa kwa gharama kubwa.

5. Mitaro katika bonde la Kinyasini imepita karibu sana na makaazi ya watu. Kutokana na hali hii Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Kilimo kuwapatia wananchi hawa elimu ya kutosha juu ya kuitunza mitaro hii muhimu kwa wakulima wetu na Taifa kwa ujumla. Uwepo wa miundombinu hii ni hatua moja kubwa ya maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

6. Kutokana na hali ya upotevu wa maji katika bonde la Chaani, Kamati inaagiza Wizara kupitia Idara ya Kilimo kuchukuwa hatua za haraka za kuirekebisha hali hii, ikibidi hata kujengwa visima ili mradi huu uweze kuwanufaisha wananchi wa maeneo husika kwa lengo la kua na uhakikaa uhakika wa chakula nchini.

7. Kamati inaiagiza Wizara kutoa Elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa miradi ambayo Serikali inawekeza kwa ajili yao. Kwa kufanya hivyo ndio tutaweza kupata uhakika wa ulinzi kwa miradi yote nchini na itawasababisha kuilinda na kuienzi miradi hiyo.

8. Kwa ujumla Kamati inaishauri Wizara kuongeza juhudi katika kuhakikisha kwamba miradi kama hii inaleta tija ili tuepukane na suala la kuagiza chakula nje.

B. Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula (Dodeani)

Mradi huu ulilenga kuondosha kabisa madhara ya Sumu Kuvu nchini, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kutekeleza miradi ya ujenzi wa maghala 14 kwa Tanzania nzima, kati ya hayo maghala mawili kujengwa Zanzibar, moja kwa upande wa Pemba na moja kwa upande wa Unguja.

Kamati kwa mara nyengine tena ilifanya ziara katika Mradi wa ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula liliopo Dodeani kisiwani Pemba baada ya kutoridhika na maendeleo ya ujenzi wa ghala hilo mwezi Machi mwaka 2022 na mwaka 2023 wakati Kamati ilipokuwa ikiendelea na kazi zake za kawaida za kutembelea miradi iliyopo chini ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

Kamati ilisikitishwa kuona kwamba Mradi huu bado haujafikia lengo lililokusudiwa. Kutokana na hali hii, Kamati iliamua kufunga safari na kwenda Tanzania Bara kwa lengo la kuonana na timu nzima ya wataalamu wa Wizara ya Kilimo ikiongozwa na Katibu mkuu pamoja na Wizara ya Kilimo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kukubaliana mambo mbalimbali likiwemo la kuusimaisha mradi huu wa Dodeani na mkandarasi achukuliwe hatua za kisheria.

Kamati ilitoa Baraka zake zote kwa Wizara zetu mbili na tunategemea taratibu nyengine zinaendelea za kuukamilisha mradi huo.

## 4.8 CHANGAMOTO ZA MRADI

1. Kamati imebaini kuwa Mkandarasi hana wataalamu muhimu (key staff) watakaoweza kuukamilisha mradi huu kwa wakati uliopangiwa.

2. Kamati pia imebaini kuwa, katika eneo la mradi hakuna vifaa vya ujenzi vya kutosha vya kukamilishia mradi huu kwa wakati, hali inayorudisha nyuma kasi ya maendeleo ya mradi. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na matofali, saruji na gypsum powder.

3. Mkandarasi hana uwezo wa kifedha wa kuendeleza mradi hadi kukamilika kwake na amejikita zaidi katika kusubiri certificate ndio ajenge.

4. Kamati ilibaini kuwa, Mkandarasi hafuati mpango kazi wake kama ilivyothibitishwa na Mhandisi Mshauri wa mradi jambo lililopelekea kutokamilika kwa wakati.

5. Kamati iliibaini kuwa Mkandarasi hafuati sheria zinazoongoza utekelezaji wa miradi kama hii pale changamoto za utekelezaji zinapojitokeza.

### 4.9 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo iwe makini katika suala zima la kupata wakandarasi wenye ujuzi na uwezo wa kifedha katika utekelezaji wa miradi kama hiyo. Aidha Wizara ifanye ufatiliaji wa karibu kwa miradi inayotoka Tanzania Bara pasi na kumuachia mkandarasi kufanya atakavyo. Kwa kufanya hivyo ndio tutafanikiwa katika mambo yetu.

## KITUO CHA UTAFITI WA MIFUGO (CHAMANANGWE -PEMBA)

Ni moja mwa vituo vya Utafiti wa mifugo viliopo chini ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar katika Wizara ya Kilimo. Kituo hiki cha kisasa kina ukubwa wa eneo wa ekeri 63 ambazo zinatumika kwa shughuli mbalimbali za taasisi.

### 4.1.1 CHANGAMOTO

1. Upatikanaji mdogo wa fedha ni tatizo linalokwamisha utekelezaji wa kazi na malengo ya taasisi hii, ikiwa ni pamoja na kukwama kwa tafiti zilizopangwa kufanyika kwa wakati. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalithibitisha hali hii, ambapo jumla ya tafiti nne zilishindikana kufanyika kutokana na tatizo hili la ukosefu wa fedha.

2. Ukosefu wa mabanda kwa ajili ya kufanyia tafiti za ng'ombe na mbuzi kunakosababishwa na ukosefu wa fedha ni changamoto nyengine, ambayo inakwamisha juhudi za kufikia malengo ya kituo hiki.

3. Kamati imebaini changamoto ya ukosefu wa ofisi katika kituo hiki, hali inayorudisha nyuma morali ya kiutendaji kwa wafanyakazi waliopo. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, taratibu za kumpata mkandarasi na michoro ya ujenzi wa ofisi hii tayari zimeshafanyika na mkandaraasi tayari ameshapatikana lakini hadi Kamati inafika katika kituo hiki, ujenzi huo bado haujaanza.

4. Upungufu mkubwa wa watafiti kituoni hapo ni changamoto inayorudisha nyuma malengo ya kuanzishwa kituo hiki. Kituo kina jumla ya watafiti 6 tu ambao ni wenye kiwango cha Cheti na Diploma.

5. Hati miliki ya eneo hili bado haijapatikana kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha.

6. Kiangazi cha muda mrefu ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati kinachosababisha uzalishaji mdogo wa malisho na kuathiri afya na uzalishaji wa mifugo.

### 4.1.2 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na umuhimu wa tafiti katika kukiendeleza kituo cha Utafiti wa Mifugo kisiwani Pemba, Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kituo kinaingiziwa fedha za bajeti kwa wakati kwa lengo la kukiwezesha kituo hiki kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

2. Kutokana na umuhimu wa kuwepo kwa mabanda kwa ajili ya kufanyia tafiti za ng'ombe na mbuzi kituoni hapo, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana kikamilifu na Wizara ya Fedha na Mipango, kuhakikisha wanawaingizia fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabanda hayo, ili ujenzi huo uweze kufanikiwa na tafiti kwa ajili ya wanyama hao ziweze kuendelea kama ilivyopangwa.

3. Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo kujenga jengo kwa ajili ya ofisi, ambalo litarejesha morali ya kiutendaji kituoni hapo.

4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma kuongeza idadi ya wataalamu kituoni hapo, kwa kuwaajiri wataalamu wenye viwango vya juu vya elimu ili, tafiti zinazopangwa ziweze kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa. Likifanikiwa hili, Kituo kitaweza kuwa mfano kwa kutoa mifugo iliyobora na wafugaji wanaofika kituoni hapo wataweza kujifunza kivitendo.

5. Wizara ya Kilimo ijitahidi kukipatia fedha kituo hiki, ili suala la upatikanaji wa hati miliki liweze kukamilika.

6. Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo kupita Kituo cha Utafiti wa Mifugo, kuongeza uzalishaji wa malisho ya wanyama katika miongo mengine isiyo ya kiangazi ili kuweza kujiwekea hakiba ya kutosha itakayoweza kutumika katika msimu wa kiangazi, ambapo hali ya uzalishaji wa malisho unaonekana kupungua kwa sababu ya jua kali.

### 4.1.3 KITUO CHA MIFUGO DONGE MUWANDA

Kituo hiki kinaratibiwa na Idara ya Maendeleo ya Kilimio kwa lengo la kupokea wanyama wote wanaotoka Bara, kuwapima pamoja na kuwaweka karantini kabla hawajaingia mitaani na watakaporidhika na usalama wao ndio hukabidhiwa cheti kwa ajili ya kwenda Sokoni au kufugwa. Hatahivyo, Wanyama wote wanaoingizwa nchini huwa na vyeti vya afya ili kuepusha kuingiza maradhi nchini.

### 4.1.4 CHANGAMOTO

1. Uchakavu wa uzio wa eneo la kuwaweka wanyama wanaoshuka bandarini hapo unaopelekea baadhi ya wanyama kutoroka na kuanza kuingia mitaani.

2. Utaratibu wa kuhifadhi nyaraka muhimu zinazoambatana na wanyama wanaowasili kituoni hapo sio rafiki. Kamati haikuridhishwa kuona nyaraka zinazagaa kituoni hapo bila ya kuwepo utaratibu wa kuziweka katika makabati.

3. Ofisi inayotumika kwa masuala ya kuratibu kituo hicho haiendani na hadhi ya kituo kwani kituo kinatumika katika ukusanyaji wa mapato lakini mazingira ya ofisi zake si rafiki kwa watendaji wake.

4. Uhaba wa vitendea kazi kama meza na viti, nafasi ya kufanyia kazi ni finyu kiasi ambacho kunakua na mkanganyiko baina ya watendaji na wahudumu wa kituoni hapo.

5. Uhaba wa watendaji wa aina zote kuanzia wataalamu hadi wahudumu na walinzi., Kamati ilipofanya ziara kituoni hapo ilishuhudia uhaba mkubwa wa wafanyakazi kulingana na wingi wa wanyama wanaofika kituoni hapo.

6. Fedha za kuendesha Ofisi (O.C) haziingii kama ilivyokadiriwa na kwa wakati , jambo linalopelekea kusuasua kwa baadhi ya shughuli walizozipangia.

### 4.1.5 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Idara ya mifugo itafute utaratibu wa kuiwekea alama mifugo yote inayowasili hapa nchini ili ijulikane kwa uwazi na kuepusha migogoro wakati wa upotevu.

2. Kamati inashauri Wizara kwa kushirikiana na Wakuu wa wilaya kuwashajihisha wananchi kuyatumia machinjio rasmi na kuachana kabisa na tatiba za kuchinja wanyama mitaani.

3. Kamati inaagiza kuandaliwa utaratibu kwa wafanyabiashara za wanyama kufanyakazi zao karibu na Wizara ya kilimo na Mifugo ili iwarahisishie kuratibu shughuli zao za mifugo kitaalamu zaidi.

4. Kamati inaishauri Wizara ya kilimo kutumia vyombo vya habari vya ndani ili kuwahamasisha wafanya biashara wa nyama na wale watu wa kawaida kujitokeza kituoni hapo na kutumia fursa ya kuchinja wanyama wao hapo kwa lengo la kuiingizia tija Serikali.

### 4.1.6 MISITU YA HIFADHI

#### Msitu wa Ngezi

Hifadhi ya Msitu wa Ngezi ni msitu wa hifadhi unaopatikana katika Kisiwa cha Pemba, Tanzania unashughulikia eneo la 1,440 hectares (3,600 acres), nyingi ikijumuisha msitu wa msingi . Hifadhi hiyo ilianzishwa mwaka wa 1959. Kijiografia hifadhi ya Ngezi iko katika ncha ya kaskazini-magharibi ya Pemba, kisiwa cha pili kwa ukubwa katika Visiwa vya Zanzibar. Inapakana na vijiji vya Kiuyu Kwa Manda (kusini), Tondooni, Verani na Makangale (kaskazini), Msuka (mashariki) na Kipangani (magharibi); upande wa magharibi, pia inapakana na Chaneli ya Pemba .

Msitu wa Hifadhi wa MaumbileNgezi ni miongoni mwa Misitu ya Hifadhi ya Serikali, ambayo ilianzishwa tangu mwaka 1955 na Serikali ya kikoloni kwa tamko la Government Notice No.31 na kuutangaza Msitu huu kuwa Msitu wa hakiba (Forest Reserve).

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1996 kupitia Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misitu nambari 10, hifadhi ya Msitu huu ilitambuliwa na kubainisha jumla ya hekta 566 zilizouzunguka msitu huu, Msitu ambao ulipandishwa hadhi rasmin na kuwa Msitu wa Hifadhi mwaka 2004. Msitu wa Ngezi uliopo kisiwani Pemba una maajabu mengi na vivutio vingi vya kitalii kimojawapo ni mti unaotowa damu ukikatwa Gamba Lake. Mti huo unajulikana kama Mdamudamu na asili yake ni India.

### 4.1.7 CHANGAMOTO

1. Kamati ilibaini changamoto ya uharibifu wa Msitu huu, unaoendelea kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na misitu kwa matumizi mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na kukata kuni, kupasua mbao na kupiga tanu za mkaa, hali inayoathiri na kupelekea upotevu wa miti mikubwa ya asili iliyomo ndani yake.

2. Motisha ndogo kwa wafanyakazi waliopo katika msitu hali inayorudisha nyuma hamu ya kiutendaji.

3. Ulinzi usio wa kuridhisha katika maeneo yote ya misitu ni changamoto inayochangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa misitu hii. Kamati imebaini kuwa walinzi waliopo katika

msitu huu ni wachache ambao hawawezi kukidhi haja iliyopo hasa tukizingatia ukubwa wa maeneo haya.  Aidha, imeelezwa kuwa, Walinzi waliopo wanakosa vifaa vya ulinzi kama vile silaha, ndege zisizo na rubani (drones) ambazo wangeweza kuzitumia katika kukabiliana na wahalifu na waharibifu wa misitu hii.

4. Idara ya Misitu imeonekana kuwa nyuma sana kiutendaji, hali inayopelekea kuwepo kwa malalamiko mengi juu ya uharibifu wa misitu yetu.

5. Usafiri ni changamoto nyengine iliyobainika. Idara ya Misitu hushindwa kutatua kesi za papo kwa papo hasa kesi za wizi na uharibifu wa misitu hii pale zinapotokezea.

6. Miundombinu ya barabara iendayo katika msitu huo haiko rafiki hasa kwa wageni kuweza kufika huko kwa urahisi.Kamati iliarifiwa kwamba wageni wanapoteza hamu ya kufika katika msitu huu, kwa sababu ya miundombinu yake kuwa mibovu na sio rafiki hasa kipindi cha mvua.

7. Kamati imebaini changamoto ya kuchelewa kwa matumizi ya mfumo wa kielekroniki katika kukusanya mapato katika misitu.

8. Changamoto ya ushirikiano mdogo baina ya jeshi la Polisi na Idara ya misitu pale wanapowapeleka wahalifu ambao wanahujumu misitu.

### 4.1.8 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu Pemba, kuendelea kushirikiana kikamilifu na viongozi wa shehia zilizozunguka eneo la misitu juu ya suala zima la kutekeleza majukumu katika kuilinda na kuhifadhi misitu kwa maslahi ya taifa.

2. Kamati inaishauri Wizara pale zinapotokezea fursa za mafunzo, wafanyakazi wa Idara ya Misitu wapatiwe mafunzo hayo kwa lengo la kuwaongezea uelewa pamoja na ari ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

3. Kamati inaiagiza Wizara kuipatia Idara hii usafiri wa uhakika kwa lengo la kuwawezesha kuzitatua kesi za uharibifu na wizi wa misitu kwa wakati muafaka.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, kuzifanyia ukarabati barabara ndogo za ndani na ile Barabara kuu iendayo katika msitu wa Ngezi, ili wageni wenye nia ya kufika Msituni hapo, waweze kufika kwa urahisi na bila ya usumbufu wa aina yoyote.

5. Kamati inaishauri Idara ya Misitu kushuka kwa jamii, kwa lengo la kuwapatia elimu na miongozo sahihi katika kuiendeleza na kuiimarisha misitu iliyopo nchini ili kuzuia kabisa uharibifu unaoendelea kufanyika na malengo ya kuwepo kwake yaweze kufikiwa.

6. Katika kuhakikisha Wizara inatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya matumizi ya mfumo wa Kielektroniki katika kukusanya mapato, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha matumizi ya mfumo huu katika misitu yote ya hifadhi wenye lengo la kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na msitu hiyo.

7. Katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi katika Misitu yote ya hifadhi wanafanyakazi katika mazingira bora na salama, Kamati inaagiza Wizara ya Kilimo, kununua vifaa vyote vya ulinzi vinavyohitajika ili waweze kukabiliana na wahalifu wa rasilimali hiyo.

### 4.1.9 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ni miongoni mwa Taasisi za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya 2019 na inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika sSheria husika.

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo inatekeleza majukumu yake katika Vituo vyake vikubwa viwili; Kwa upande wa Unguja, kituo kipo Mbweni – ambapo hapo ndio Makao Makuu ya WAKALA, na kwa Pemba, Kituo kipo Wawi.

Eneo la WAKALA la Mbweni Unguja lina ukubwa wa hekta 2.91 (Ekari 7.25) na lile la Wawi Pemba lina ukubwa wa mita za mraba elfu nne na mia saba (4700m2), sawa na wastani wa ekari 1.25.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo unaongozwa na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (Zanzibar Vision 2020), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA III), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Mipango Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi wa Sekta ya Kilimo (ATI), Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Zanzibar - ZASDP (2019 – 2029), ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020, pamoja na Sheria na Sera mbali mbali za Wizara.

### 4.2.1 CHANGAMOTO

1. Uhaba wa matrekta unaozorotesha shughuli za uandaaji wa mashamba kwa ajili ya ukulima, Wakati Kamati imefanya ziara kwa wakala imekuta jumla ya matrekta 38 kwa Unguja na Pemba ambayo ni mazima na jumla ya matrekta 14 yanahitaji matengenezo.Uhaba huu wa matrekata husababisha wakulima wengi kutopata huduma ya matrekata kwa wakati sahihi na kupelekea kutolima kwa wakati.

2. Matrekta yanayoharibika kuchelewa kufanyiwa matengenezo kutokana na karakana ya Wakala kuhamishiwa kwenda Karakana Kuu ya Magari na kupelekea gharama kubwa za utengenezaji wa matrekta pamoja na kuchukua muda mrefu wa matengenezo tofauti na hapo awali kitengo cha ufundi matrekata kilipokuwepo chini ya Wakala wa matrekta

ambapo shughuli zote za utengenezaji wa matrekta zilikuwa zinafanyika kwa wakati na kwa gharama nafuu.

3. Baadhi ya matrekta kutofanya kazi kwa ufanisi na mengine kutoingia kabisa katika mabonde ambayo yamewekwa miundombinu mipya ya umwagiliaji kutokana na miundombinu hiyo kutozingatia aina ya matrekata tuliyonayo. Kwa mfano uwepo wa njia nyembamba katika mabonde yenye mradi wa umwagiliaji kunasababisha baadhi ya matrekta kushindwa kufika katika mashamba hayo hali inayopelekea wakulima kukosa huduma stahiki na Wakala kukosa mapato.
4. Kutoingia kwa wakati fedha za ruzuku na za matumizi ya kawaida (OC) jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za Wakala katika kufanya matengenezo ya matrekta na shughuli mbalimbali za uendeshaji wa ofisi za Wakala.

### 4.2.2 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ili huduma za matretka ziweze kuimarika ni vyema Wakala kuongeza idadi ya matrekta mapya kwa vile idadi iliyopo sasahivi haitoshi kuhudumia wananchi wote kwa wakati mmoja jambo ambalo linakwamisha juhudi za wakulima wetu katika kilimo cha mpunga. Aidha Kamati inashauri Wakala kuharakisha kuyafanyia matengenezo matrekta 14 ambayo yameharibika ili kuanza kufanya kazi na kupunguza changamoto ya uhaba wa matrekta ambayo Wakala inakabiliana nayo kwa sasa.
2. Kamati inashauri Serikali kukirudisha kitengo cha ufundi wa matrekta kuwa chini ya Wakala ili kurahisisha shughuli za utengenezaji wa matrekta kwa wakati na kwa gharama nafuu ambapo kwasasa matrekta yaliyoharibika yanachukua muda mrefu kutengenezwa na kufanyiwa matengenezo kutokana na urasimu uliopo katika Karakana kuu ya Magari
3. Ushirikishwaji wa wakala katika miradi mbalimbali ni jambo muhimu litakaloleta ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inashauri Wizara ijenge utaratibu wa kuwashirikisha wataalamu kutoka ofisi ya Wakala wa matrekta katika utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji ili kutoa mapendekezo ya namna gani miundombinu hiyo iweze kuendanana utoaji wahuduma za matrekta.

4. Aidha, Kamati inashauri Wakala kununua matrekta yatakayoweza kuendana na miundombinu iliyowekezwa katika miradi ya umwagiliaji ili shughuli zote za uandaaji wa mabonde pamoja na kilimo cha umwagiliaji kifanyike kwa ufanisi mkubwa.

5. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha ruzuku na fedha ya matumizi ya kawaida (OC) inatolewa kwa wakati na kwa kiwango kilichopangwa ili kuwezesha Wakala kuendeleza shughuli zake kwa ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na kununua vipuri vya matrekta na kuweza kuyafanyia matengenezo matrekta yaliyoharibika kwa lengo la kuwahudumia ipasavyo wakulima wetu.

### 4.2.3 IDARA YA UMWAGILIAJI

### 4.2.4 CHANGAMOTO

1. Uhaba wa fedha za matumizi ya kawaida (OC) kwa idara ya umwagiliaji maji unarudisha nyuma ufanisi wa utendaji kazi wa idara hii, ambapo kwa kipindi cha julai-Disemba, 2023 Idara imepangiwa kutumia jumla ya Tzs 235,393,125 na kupokea jumla ya Tzs 60,069,140 sawa na asilimia 25.5 kwa kipidi hicho.

2. Ufinyu wa Ofisi ya Idara ya umwagiliaji, Kamati imebaini idara kuwa na jengo la kizamani, ambalo halina ghaiba nzuri pamoja na uchakavu wa vitendea kazi vya Afisi.

### 4.2.5 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha fedha ya matumizi ya kawaida (OC) inatolewa kwa wakati na kwa kiwango kilichopangwa ili Idara itekeleze shughuli zake za kawaida kama ilivyojipangia katika bajeti husika.

2. Kamati inashauri Wizara kuliboresha jengo la Idara ya Umwagiliaji ili kuwa la kisasa na lenye ghaiba nzuri kwa lengo kuboresha mazingira mazuri ya kazi kwa watendaji wake, aidha kuongeza idadi ya vyumba vya Ofisi na vyumba vya mikutano.

### 4.2.6 AFISI YA AFISA MDHAMINI

Katika mzunguko wake wa kwanza, Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ilitembelea ofisi ya Afisa Mdhamini wa Wizara yaKilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba.

### 4.2.7 CHANGAMOTO

1. Uchache wa Watendaji ambapo Ofisi haina wafanyakazi wa kutosha wakuweza kukidhi mahitaji ya wakulima na wafugaji jambo ambalo linalopekea wakulima wetu kupata tabu sana. Vipando na mifugo yao inakosa usimamizi na ushauri mzuri kutoka kwa wataalamu ambao ndio adhma ya kuanzishwa kwa Wizara hii.
2. Kuibuka kwa maradhi ya mifugo ambayo hayajapatiwa kinga wala tiba yake yanayopelekea kupoteza mifugo mingi na kurejesha nyuma juhudi za wafugaji nchini.
3. Wizara kwa Upande wa Pemba kukosa usafiri kwa ajili ya matumizi ya Ofisi pamoja na kutekeleza shughuli za ufuatiliaji nje ya ofisi.
4. Ukosefu wa mbolea kwa wakulima wengi unaopelekea kushindwa kuendesha shughuli zao za kilimo kwa ufanisi kwani imebainika kuwa mbolea inauzwa kwa bei ya juu tofauti na uwezo wa wakulima wetu.
5. Kamati imebaini kuwa pamoja na sera mbalimbali zilizowekwa na Serikali kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula, bado nchi yetu haijafanikiwa katika utekelezaji wa sera hizo. Suala hili linapelekea athari ya kiuchumi Serikali hulazimika kuingiza fedha nyingi kwa Wizara hii kwa lengo la kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, ununuzi wa pembejeo ili tuweze kuondokana na tabia ya kuagiza chakula nje ya nchi.
6. Uharibifu wa misitu unaosababishwa na shughuli zinazofanywa na binaadamu unaopelekea kupungua kwa miti ya asili kwenye misitu yetu
7. Uchangiaji wa shilingi 60,000 kwa ajili ya huduma ya kusafishiwa shamba ni jambo linalowakwaza sana wakulima kutokana na ukweli kwamba wakulima hao hawawezi kuchangia gharama hizo na kupelekea mashamba mengi kukosa huduma hiyo.
8. Upatikanaji wa miche ya mikarafuu bado ni changamoto kwa wakulima ambapo hadi sasa Wizara haijafanikiwa katika uzalishaji wa idadi ya miche iliyopangwa.

### 4.2.8 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa watendaji, Kamati inaishauri Serikali kuipatia watendaji wanaohitajika Wizara ya Kilimo kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake.
2. Kamati inaishauri Wizara kutafuta suluhisho la kudumu la ukosefu wa mitaji kwa wakulima pamoja na wafugaji wetu kwa kuwaunganisha na Taasisi za kifedha ili wapatiwe mikopo nafuu itakayowawezesha kulipa kwa wakati na kutimiza malengo yao waliyojiwekea.
3. Kamati inaiagiza Wizara izidishe bidii katika kuendeleza utaratibu wa kuwapatia Wafugaji chanjo pamoja na dawa na kubaini changamoto zinazowakabili wanyama wao ili kuondokana na majanga yanayowakabili wafugaji wetu.
4. Kamati inaiagiza Wizara, kuipatia usafiri wa uhakika Ofisi ya Afisa Mdhamin kwa ajili ya kusaidia katika utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli zake nje ya ofisi.
5. Ili kufanikisha upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wetu, Kamati inashauri usimamizi wa mbolea bado ubakie chini ya mikono ya Serikali ili iweze kuuzwa kwa bei rafiki na hatimae wakulima kuweza kuimudu na kupelekea kurahisisha kilimo chao.
6. Kamati inaishauri Wizara ya kilimo kuanzisha mkakati maalumu wa kupambana na uhaba wa chakula nchini na mkakati huu uanzwe katika ngazi ya Shehia, Wilaya hadi Mkoa ili kujua changamoto zinazowakabili wakulima na hatimae kuwawezesha kuengeza uzalishaji hapa nchini ikiwa pamoja na kuwaunganisha katika Taasisi za kuwawezesha wananchi kiuchumi.
7. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Kamati za Ulinzi za Wilaya na Mkoa ili kuhakikisha ulinzi katika misitu yetu na kwa wale watakaobainika kufanya shughuli za kijamii katika misitu hiyo ambazo zinapelekea uharibifu basi wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria.
8. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inatumia miongoni mwa mashamba yake kwa lengo la kuotesha miche mipya na kuwakabidhi wakulima ili zao la karafuu liweze kurudi katika ubora wake na kuzidisha mapato nchini.

### 4.2.9 MACHINJIO YA WANYAMA

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara yake katika chinjio la wanyama Mkoani kisiwani Pemba na Donge Muwanda kwa upande wa Unguja, kwa lengo la kuangalia hali halisi ya machinjio hayo. Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo kwa kiasi kikubwa zinakwamisha utekelezaji wa shughuli za kila siku katika machinjio hayo.

### 4.3.1 CHANGAMOTO

1. Kwa upande wa chinjio la Mkoani Pemba, Kamati ilijionea eneo linalotumika kama machinjio ya wanyama ambalo kiuhalisia ni eneo dogo na limekosa vigezo, hasa upande wa miundombinu kwa utekelezaji wa shughuli za uchinjaji wa wanyama hao. Kamati iliarifiwa kwamba, maeneo hayo yana uwezo wa kuchinja ng'ombe hata wawili kwa wakati mmoja, hali inayopelekea serikali kukosa mapato ya uchinjaji hasa kwa siku za msimu wa sikukuu za kitaifa, ambapo wananchi wengi huhitaji huduma hii lakini hushindwa kulitumia chinjio hilo na badala yake huishia kuchinja wanyama hao katika sehemu zisizo rasmi.

2. Kamati pia ilibaini changamoto ya ukosefu wa ngoweko *'hooks'* za kuwekea nyama kwa lengo la kuiacha nyama ijichuje damu hali inayowalazimu wachinjaji kuiweka nyama hiyo juu ya baraza jambo ambalo ni hatari na si utaratibu unaofaa.

3. Kukosekana kwa uzio katika chinjio la Mkoani kwa kuhifadhia wanyama hali inayopelekea wanyama hao kuzurura katika makaazi ya watu.

4. Kamati imebaini uweopo wa hali hatarishi kwani imegundua kua maji yamejaa katika shimo linalotumika kuhifadhia mabaki na viungo visivyohitajika kwa wanyama wanaofika kuchinjwa katika eneo hilo. Pia changamoto nyengine ambayo wafanyakazi katika chinjio hili hulazimika kufanya kazi ya ziada kwa kukusanya mabaki hayo katika sehemu isiyo rasmi jambo linahatarisha afya za wafanyakazi hao pamoja na wananchi wetu kwa ujumla.

5. Uchafu pamoja na harufu mbaya katika chinjio la Mkoani ni hali inayoweza kuathiri afya za wananchi hasa tukizingatia kwamba, chinjio lipo karibu sana na eneo ambalo wavuvi hulitumia katika shughuli za kujitafutia riziki zao.

### 4.3.2 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuanzisha mradi maalumu wa kuweka chinjio kubwa na la kisasa kisiwani Pemba kwa lengo la kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

2. Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutafuta vifaa vyote muhimu vinavyohitajika katika machinjio yaliyopo hivi sasa kisiwani Unguja na Pemba kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku pamoja na kuiweka nyama inayochinjwa katika hali ya usafi na usalama.

3. Kamati inaiagiza Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuharakisha uwekaji wa huduma ya umeme katika chinjio la Mkoani ili kuwawezesha watendaji wetu kuweza kutekeleza majukumu yao muda wowote pale inapohitajika.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagilaiji, Maliasili na Mifugo kuongeza idadi ya matenki yenye ujazo mkubwa wa kuhifadhia maji katika machinjio yaliyopo nchini kwa lengo la kumaliza kabisa changamoto ya maji iliyopo katika maeneo hayo.

5. Kamati inaishauri Wizara kuweka uzio madhubuti katika machinjio yaliyopo kwa lengo la kuwahifadhi wanyama wanaofika kuchinjwa katika maeneo hayo.

6. Ili kulinda afya za watendaji wa machinjio na walaji wa vitoweo, Kamati inaagiza Wizara ya Kilimo kutafuta sehemu maalumu ya kutupa mabaki yasiyohitajika yatokanayo na wanyama wanaochinjwa.Kadhalika, tunaiomba Wizara kupitia Idara ya Mifugo kudumisha usafi katika machinjio yetu ili kuziweka salama afya za watumiaji na wanachi kwa ujumla.

7. Kutokana na umuhimu wa utaratibu wa kawaida uliowekwa kwa wanyama kuwekwa kituoni kwa muda wa masaa ishirini na nne hadi kuchinjwa, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuendelea na utekelezaji wa utaratibu huo kwa lengo la kumlinda mtumiaji na kumuepusha na maradhi.

## SEHEMU YA TANO

### 5.1 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

### 5.2 IDARA ZA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Sera na Utafiti
3. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko
4. Idara ya Maendeleo ya Viwanda
5. Afisi ya Afsa Mdhamini Pemba.

### 5.3 TAASISI NA MASHIRIKA YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

1. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)
2. Wakala wa Usasjili wa Biashara na Mali
3. Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC)
4. Taasisi ya Viwango zanzibar (ZBS)
5. Mamlaka ya Usimamizi wa leseni
6. Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, vidogo na vya Kati (SMIDA)
7. Tume ya Ushindani Halali wa Biashara
8. Baraza la Ushindani wa Biashara
9. Wakala wa Vipimo.

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Biasharana Maendeleo ya Viwanda imepanga kutekeleza vipaumbele katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kuendeleza Ujenzi kwenye eneo la Maonesho ya kibiashara Dimani; Kuratibu ujenzi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano (Convention Centre); Kujenga Vituo

Jumuishi kwa ajili ya Urasimishaji Biashara, na kuyaendeleza Maeneo ya Viwanda ya Dunga na Chamanangwe.

### 5.4 UKUSANYAJI WA MAPATO

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kukusanya jumla ya Tzs. bilioni 1.750kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa huduma zinazotolewa. Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya Tzs. milioni 490.69zilikusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo ni sawa na asilimia 61 ya makadirio yamakusanyo. Aidha, Baraza la Udhibiti Mfumo wa Utoaji Leseni (BLRC) lilipanga kukusanya jumla ya Tzs. milioni 32.97 kutoka katika Mamlaka za Serikali.

Zinazotoa leseni, hadi kufikia Disemba 2023, Baraza limekusanya Tzs. milioni 42.02kutoka katika mamlaka hizo ambazo zimeingizwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kwa upande wa matumizi, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Biasharana Maendeleo ya Viwanda ilipangiwa kutumia jumla ya Tzs. bilioni 35.952kwaajili ya kutekeleza programu zake kuu tatu (3). Hadi kufikia Disemba 2023, jumla ya Tzs. bilioni 10.930zimetumika sawa na asilimia 64.

### 5.5 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Kamati ilifanya ziara ya kutembelea kituo cha ununuzi wa karafuu Wete na kupata nafasi ya kuonana na watendaji wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ambao wanatoa huduma katika kituo hicho na kupatiwa taarifa inayohusiana na shughuli zote zinazofanyika kituoni hapo. Shughuli hizo ni pamoja na kupokea karafuu zinazofika kituoni hapo, kuchekecha, kupima na hatimae kununuliwa na Shirika. Kamati pia ilipata nafasi ya kuzungumza na wafanyabiashara waliofika kituoni hapo kuuza karafuu zao kwa lengo la kujua changamoto zinazowakabili wafanyabiashara hao ili kutatua changamoto hizo.

Kwa upande wa Tanzania Bara, Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara katika Shirika la Biashara la Taifa **Tawi la Dar es Salaam.** Tawi hilo lina jumla ya wafanyakazi saba na linaloongozwa na Meneja wa Tawi. Kamati ilibaini changamoto ambazo zikiweza kutatuliwa zitalisaidia tawi kuendelea na shughuli zake kwa ufanisi mkubwa. Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni kama zinavyoonekana katika taarifa hii.

### 5.6 CHANGAMOTO

1. Wakulima wengi hawana taaluma nzuri juu ya utaratibu wa kupunguza unyevu katika karafuu zao na hali hii inasababisha malalamiko mengi kutoka kwa wakulima pale ambapo wanapotajiwa grade au kiwango cha karafuu zao kuwa ni za chini kutokana na kuwa na mnyevu.

2. Wananchi bado hawana taaluma nzuri juu ya machine ya kuchekechea karafuu ambazo zimefungwa katika vituo vyote vya kununulia karafuu Zanzibar kwa lengo la kupata bidhaa iliyo bora. Wakulima bado wanaimani kua machine hizo

hazifanyi kazi vizuri kwakua zinabakisha chenga nyingi sana na kupelekea kupungua kwa ujazo wa karafuu zao ambazo wamezifikisha vituoni kwa mauzo.

3. Wafanya biashara wasiokua na uzalendo wa nchi hii, wanaitumia fursa ya kuomba magunia kutoka ZSTC yenye chapa ya shirika na kutia karafuu zao na hatimae kuziuza kwa magendo nje ya nchi.
4. Baadhi ya wananchi kutokubaliana na mfumo wa malipo kwa kutumia akaunti za benki na mitandao ya simu  na kuleta usumbufu kwa watendaji wa Shirika katika kuwapatia malipo yao.
5. Uchache wa watendaji wa kudumu kwa baadhi ya vituo wakati wa manunuzi unapelekea kukiukwa kwa baadhi ya taratibu za manunuzi katika upimaji, upasishaji na uchungaji.
6. Utaratibu wa kutumia vyeti vya sheha ili kuthibitisha uhalali wa umiliki wa karafuu bado ni changamoto kwani unaweza kukuta karafuu zinatoka Shehia nyengine na muhuri wa sheha unapigwa shehia nyengine hii inaleta usumbufu kwa Shirika katika kuweka kumbukumbu sahihi za uzalishaji wa karafuu kiwilaya na pia katika kufanya malipo ya ununuzi wa karafuu hizo.
7. Kutochukuliwa hatua za kisheria wanaokamatwa na magendo ya karafuu ni jambo linalokwaza juhudi za Serikali kukomesha biashara hiyo haramu na kupelekea zoezi la ukamataji wa magendo kua gumu zaidi.
8. Shirika kukosa usafiri kwa ajili ya kutekeleza shughuli zake za ufuatiliaji nje ya ofisi kwa upande wa tawi lake la Dar-es-salaam.
9. Kukosa kuendelezwa kwa nyumba ya Shirika iliyopo maeneo ya Sinza na ambayo inakabiliwa na changamoto ya kuingia maji kipindi cha mvua kunaipunguzia thamani nyumba hiyo.
10. Ufinyu wa Ofisi ya Tawi la Dar-es-salaam unapeleekea Shirika kutokuwa na mazingira bora ya kufanyia kazi.

11. Bidhaa zinazouzwa na duka la Shirika lililopo Dar-es-salaam haziendi sambamba na majukumu ya Shirika kwani baadhi ya bidhaa zilizomo ni za kuagizwa kutoka nje ya nchi na ambapo ingelikuwa ni busara kuwekwa kwa bidhaa za ndani pekee ikiwemo mafuta ya mimea, sabuni n.k

12. Kamati imebaibni kupungua kwa uzalishaji wa karafuu kunasababishwa na tabia za watu kuharibu mazingira kwa kukata miti ovyo hususani miti ya mikarafuu na kufanya kuni na mkaa ingawa Shirika limeripoti kuwa kupungua kwa uzalishaji wa karafuu kunatokana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

13. Baadhi ya watumishi ambao sio waaminifu kutoka katika vyombo vya ulinzi na usalama wanashirikiana na watu wa magendo katika kusafirisha karafuu nje ya nchii na ndio jambo linalopelekea karafuu zinazokamatwa kutopatikana wenyewe.

14. Kwa muda mrefu, Wizara ya Biashara ilikua ikitenga fedha na kuziwasilisha Wizara ya kilimo ili kuandaa miche ya mikarafuu kwa lengo la kuwapatia wakulima na kuongeza uzalishaji wa karafuu nchini. Utaratibu huo haukuwa na mafanikio na kupelekea Wizara kuusitisha na badala yake kuwapatia wakulima vifaa mbalimbali.

15. Task force iliyoundwa kwa ajili ya kupambana na magendo ya karafuu bado haijaweza kusaidia Serikali hasa ikizingatiwa kuwa bado magendo yanaendelea siku hadi siku.

16. Kiwanda cha Makonyo bado ni mzigo kwa Shirika na hakifanyi kazi kama yalivyo matarajio ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

## 5.7 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kukaa na wakulima wa karafuu ambao ndio wadau wao wakuu kwa lengo la kuwapa Elimu juu ya masuala mbali mbali yanayohusiana na zoezi zima la ununuzi ikiwemo matumizi ya machine ya kuchekechea, mizani za kupimia na hata umuhimu wa kuwepo kwa kifaa cha kupimia unyevu wa karafuu

pindi zikifika kituano hapo. Hii itajenga ukaribu na kuaminiana baina ya watendaji wa kituo na wakulima na kupelekea mwendelezo mzuri wa zao letu hili.

2. Kamati inalishauri Shirika kuendelea kuwaelimisha wateja wake umuhimu wa kukubali kupokea malipo yao kwa njia ya benki au ya simu kwani kunarahisisha zoezi la ulipaji pamoja na kupelekea usalama wa fedha zao.
3. Kamati inalisisitiza Shirika kujipanga kwa kuwa na watendaji wa kutosha katika vituo vya kununulia karafuu hasa kipindi cha manunuzi ya karafuu ili kupunguza kasoro zinazojitokeza wakati mchakato huo unapofanyika.
4. Kamati inaiagiza Serikali kusimamia ulipaji wa fidia kwa wale wanaopata ajali katika mikarafuu na kuhakikisha fedha hizo zinawafika wahusika kwa wakati pamoja na kifuta jasho kwa wachukuzi ambao wanatumikia maeneo yote ya vituo vya uuzwaji wa karafuu.
5. Kamati inaishauri Wizara kuipatia watendaji wanaohitajika na Shirika la ZSTC kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake katika matawi yake yote.
6. Kamati inaishauri Wizara kuitafutia Shirika Ofisi ya kudumu na yenye nafasi ya kutosha na mazingira mazuri kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yake ya kibiashara Tanzania Bara.
7. Kwavile Duka liliopo katika Tawi la Dar es Salam halina tija na ni mzigo kwa Shirika, Kamati inaliagiza Shirika kulifunga duka hilo na kutafuta mradi mwengine ambao utaweza kutuingizia mapato Serikali ambao unaendana na kazi za Shirika lenyewe.
8. Kamati inaishauri Wizara kuitafutia Shirika Ofisi ya kudumu na yenye nafasi ya kutosha na mazingira mazuri kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Shirika.

9. Kamati inaishauri Wizara kutafuta muwekezaji ili Nyumba iliyopo Sinza ivunjwe na kuanzishwa mradi mkubwa kama vile ujenzi wa Gorofa lenye nyumba za kukodisha au ujenzi wa maegesho ya kisasa ili kuzalisha faida kubwa.

10. Kamati inashauri kiwanda cha makonyo kifanyiwe matengenezo makubwa ili kwenda sambamba na kasi ya Mheshimiwa Rais ya kuleta maendelea ya viwanda nchini. Kuboreshwa kwa kiwanda hiki kitaliwezesha Shirika letu yetu kuzidisha uzalishaji na hatimaye kuchangia kwenye ukuwaji wa pato la Taifa.

11. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutafuta biashara mbadala ambayo itaweza kusaidiana na zao la karafuu kunyanyua uchumi wetu. Mkakati huu wa kuanzisha biashara nyengine utasaidia pia kukabiliana na madeni ambayo Shirika inakabiliana nayo.

12. Shirika liendelee kujitangaza kimataifa pamoja na kutumia vyombo vyetu vya ndani kwani biashara ni matangazo na Shirika letu ni miongoni mwa mashirika yaliojikita katika masuala mazima ya Biashara nchini ikizingatiwa kuwa zipo nchi za visiwa ambazo pia zinazalisha karafuu na kuuza katika soko la dunia.

13. Kwa ajili ya kupambana na magendo ya karafuu, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kubadili utaratibu wa kuwapata wajumbe wa kamati ya ulinzi (task force) kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wajumbe katika kamati hiyo hawatekelezi majukumu yao ipasavyo.

14. Kamati imelipongeza Shirika kwa kutanua wigo wake hasa pale ilipoamua kwenda kuengeza mtaji kwa kununua karafuu Tanzania bara ili ihakikishe karafuu hizi haziendi kuharibu brand yetu ambayo tumeipata baada ya kazi kubwa kufanyika.

## 5.8 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya viwango ya Zanzibar Namb. 1 ya mwaka 2011. Katika kuimarisha na kuengeza nguvu katika suala zima la upimaji bidhaa ZBS kwa makusudi iliamua kuengeza baadhi ya

maabara kama vikle maabara ya Nguo na Ngozi, maabara ya vimalea pamoja na maabara ya vifungashio ambazo hazikuepo hapo mwanzoni. Katika ziara Kamati ilijionea utendajikazi wa Taasisi hii na kuridhishwa kutokana na kutekelezwa vyema kwa ilani ya Chama cha mapinduzi ya mwaka 2020-2025 ibara ya 157D , E na G kwa madhumuni yale yale ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi. Kamati pia ilipata nafasi ya kwenda katika taasisi inayofanana na hii huko Tanzania bara TBS kwa lengo la kujifunza ili iweze kuisaidia taasisi hii katika masuala mazima ya uendeshaji pamoja na utekelezaji wa Ilani.

Kamati iliarifiwa kuwa, ujenzi pamoja na kazi ya kuchimba mashimo kwa ajili ya kusimika mashine imekamilika na kontena za vifaa vitakavyotumika kufanyia shughuli zote katika mradi huo zimeshawasili bandarini na mradi unatarajia kukamilika mwezi wa Februari 2024. Kamati iliridhika na maendeleo ya ujenzi huo wa kituo cha ukaguzi wa vyombo vya moto pamoja na kituo jumuishi 'one stop center' chenye lengo la kuwapunguzia usumbufu wananchi pindi wanapofika kituoni hapo kupatiwa huduma za upimaji, ukaguzi na sehemu za ofisi ya taasisi za kifedha ambazo zitahusika na malipo.

Kamati ilipata bahati ya kutembeleaTaasisi ya Viwango Tanzania (TBS) na imebaini kuwa, pamoja na ukubwa wa Taasisi hiyo bado inapata msaada kutoka Serikali kuu kama vile mishahara, miradi mbali mbali na mambo mengine yote ambayo Taasisi nyengine za Serikali zinafaidika nayo.

## 5.9 CHANGAMOTO

1. Kamati imebaini kwamba Taasisi ya ZBS sio mwanachama wa Jumuiya Taasisi za Viwango za Afrika mashariki pamoja na ile ya Afrika kwa ujumla. Kwa mnasaba huo, ZBS inashiriki vikao vya Nchi wanachama kama waangalizi tu.

2. Ucheleweshaji wa kuanza kazi mradi wa ukaguzi wa vyombo vya moto kutokana na kukwama kwa kontena za vifaa vinavyotarajiwa kutumiwa na Taasisi hii kwa kukosa msamaha wa kodi. Kuendelea kukwama bandarini kwa kontena hizo kutapelekea kuzoorotesha maendeleo ya Taasisi hii na Serikali kwa ujumla.

3. Kukosekana kwa wakaguzi wa kutosha katika maeneo ya bandari, masoko, maghala na kukagua wajasiriamali pamoja na maeneo yote yenye viwanda kunakopelekea kupotea kwa mapato.

4. Ukosefu wa maabara ya Metrolojia inayohusiana na uhakiki vifaa vinavyotumika kupima "Mass, Volume, Temparature na Pressure" unaosababisha ukosefu wa mapato kwa Serikali kila mwaka.

5. Kamati Ilielezwa kuwa Wajasiriamali wengi wanakiuka masharti ya kupatiwa leseni ya ubora kwa vile wanashindwa kuendelea na uzalishaji mara tu wanapopatiwa alama ya ubora, hali inayorudisha nyuma juhudi za Taasisi hii.

6. Wanachi kua na uelewa mdogo juu ya kuitambua miongozo inayotolewa na ZBS katika uzalishaji wa bidhaa zao jambo ambalo linakwamisha juhudi za ZBS katika kupata bidhaa zenye ubora na viwango Nchini.

### 5.1.1 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Viwanda kuharakisha mchakato wa kuendelea kuboresha maabara za ZBS ili ziweze kuwa na viwango vinavyokubalika kwa lengo la kuiwezesha Taasisi yetu hii kuwa mwanachama kamili kama ilivyo Taasisi ya viwango Tanzania. Kamati inaishauri Serikali kuipa Baraka zote Taasisi ya ZBS ili ianze mchakato na maandalizi ya kujiunga na uwanachama katika jumuiya mbalimbali za kikanda na bara la Afrika.

2. Kamati pia inaishauri Taasisi ya ZBS kutafuta wadau wa maendeleo kama vile UNDP na wengine ili iweze kujiongezea taaluma kwa watendaji wake kwa lengo la kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

3. Aidha, Kamati inaishauri Taasisi ya ZBS kujenga tabia ya kuandaa maandiko au miradi ambayo itawasaidia kupata wafadhili kwa lengo la kuzidisha mapato kwa Taasisi na kupunguza utegemezi kwa Serikali kuu.

4. Kamati inaiagiza Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kujitangaza kwa wananchi pamoja na kutoa elimu kuhusiana na umuhimu wa Taasisi hii, kufanya hivyo kutasaidia kutambulika kwa Taasisi pamoja na kuongeza uelewa wa wananchi ambao wengi wao hawajui umuhimu wa Taasisi hii na badala yake baadhi ya wajasiriamali wanakiuka masharti ya kupatiwa leseni ya ubora.

5. Kamati inaiagiza Wizara kuharakisha ununuzi wa vifaa vya maabara ya metrolojia kwa lengo la kuboresha maabara zetu.

6. Kutokana na tulichojifunza kwa Taasisi ya Viwango Tanzania (TBS), tunaishauri Serikali kutafuta mfumo mzuri wa kuijengea uwezo Taasisi yetu ya viwango Zanzibar (ZBS)ili kufanya kazi kwa ufanisi na kuweza kufanya marudisho (gawio) kwa wakati kama ulivyopangiwa na Serikali kuu.

### 5.1.2 TAASISI YA USAJILI WA HAKIMILIKI (COSOZA).

Taasisi ya msajili wa Hakimiliki ina jukumu la kusimamia Sheria ya Hakimiliki na. 14 ya mwaka 2003 ambayo imejikita zaidi katika kusajili,kukusanya na kugawa mirabaha kwa wamiliki husika wa hakimiliki. Taasisi hii imepewa jukumu na wabunifu pamoja na watunzi katika suala zima la kusimamia haki zao chini ya usimamizi wa pamoja na hakimiliki (CMO).Aidha, COSOZA inatekeleza majukumu mengine kisheria kama vile kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, wasanii, watayarishaji wa kanda za sauti, wachapishaji na watangazaji pamoja na mambo mengine yanayohus8iana na hayo.Hatahivyo, kwa Tanzania masuala ya Milki bunifu yanasimamiwa na mamlaka mbili huru za kisheria kwavile milki bunifu sio masuala ya Muungano.

### 5.1.3 CHANGAMOTO

1. Uhaba wa wafanyakazi, Licha ya kupitishwa kwa Muundo wa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Lakini bado kumekuwa na Ugumu wa kupatiwa wafanyakazi ikiwa kwa uhamisho au kupatiwa kibali cha uajiri.

2. Uchakavu na Ukosefu wa Samani (furniture) pamoja na vitendea kazi, kama vile Computers, Printers, Laptops, ambazo ni msingi wa utendaji kazi wa Afisi.

3. Uhaba wa Upatikanaji wa Fedha zilizopangwa kwaajili ya utekelezaji wa shughuli za Afisi (OC) ambayo huikosesha Taasisi fursa ya kufanya malipo yanayoikabili Jumuiya ambazo Afisi ni mwanachama ikiwemo CISAC (Confideration of Societies of Authors and Composers) na IFRRO (means International Federation of Reprographic Rights Organization).

4. Uhaba wa vyombo vya usafiri. Kwa sasa Afisi ina gari moja tu ambayo inatumika kwajili ya matumizi ya Afisi pamoja na matumizi ya kukusanya mirabaha jambo ambalo linasababisha kutumia muda mrefu na kupelekea kusimama kwa shughuli nyengine za Afisi.

5. Ufinyi wa Ofisi ndani ya Taasisi. Kamati ilipotembelea COSOZA ilikosa hata nafasi ya kukaa kwavile eneo walilotengewa kama ofisi ni dogo na haliruhusu kupokea wageni wengi kwa wakati mmoja.

### 5.1.4 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kuipatia watendaji wanaohitajika na Taasisi kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu yake.

2. Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kubadili utaratibu wa kuingiza O.C kwani uwepo wa fedha hizo za uendeshaji Ofisi huisaidia Taasisi kuweza kufanya makusanyo yake, kulipa stahiki kwa wadau wake ambao ni wasanii pamoja na kuweza kulipa ada ya uanachama katika jumuiya mbali mbali ambazo COSOZA ni mjumbe.

3. Kamati inaishauri Wizara kuitafutia Taasisi Ofisi ya kudumu na yenye nafasi ya kutosha na mazingira mazuri kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi kwani mazingira ya sasa si rafiki kwa utendaji wa shughuli za kila siku za Taasisi.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kuipatia COSOZA samani (furniture) ili iweze kuratibu shughuli zake kwani Kamati ilishuhudia upungufu wa samani kwa Taasisi hiyo wakati wa ziara yake.

5. Kamati inashauri Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kuipatia usafiri Taasisi hii ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kupunguza upotevu wa mapato ya Serikali kwani kutokua na gari ya ufuatiliaji wa makusanyo kunaviza majukumu yao ya kuinua hali za wasanii nchini.

### 5.1.5 KIWANDA CHA MWANI

Kamati ilifanyaziara katika kiwanda cha kusarifu mwani kilichopo Chamanangwe na kujionea hatua zinazoendelea za ujenzi wa kiwanda hicho ambapo shughuli za ujenzi wa kiwanda zimekamilika kwa asilimia kubwa na hatua inayofuata ni kusubiriwa kuwasili kwa mashine za kuendeshea kiwanda. Kamati imeridhika kwa hatua hiyo pamoja na viwango vya miundombinu vilivyoekwa katika kiwanda hicho. Kuanza kazi kwa kiwanda hiki kutasaidia sana wakulima wa mwani kupata bei nzuri na soko la uhakika la bidhaa yao ambayo ndio malighafi ya kuzalisha bidhaa mbalimbali.

### 5.1.6 CHANGAMOTO

1. Kamati imebaini kuwa miundombinu ya maegesho ya magari pamoja na sehemu za kupokelea malighafi zitakazowasili kiwandani hapo haiko katika hali nzuri. Kadhalika, eneo la nje ya kiwanda bado halijawekwa katika hali nzuri kwani pindi ikinyesha mvua hakuna shughuli itakayoweza kufanyika kiwandani hapo kutokana na tope na maji yanayotuama katika maeneo hayo.

2. Ucheleweshaji wa kutiliana saini kwa makubaliano baina ya Serikakli ya mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya Uingereza juu ya suala zima la uendeshaji wa kiwanda hicho bado ni changamoto iliyobainika kupitia kwa Kamati, kwani hadi sasa ni mzunguko wa pili kamati inatembelea eneo hilo na kubaini bado mkataba huo wa makubaliano ya uendeshaji haujaekwa saini tofauti na matarajio yetu.

3. Ofisi ambazo zitatumika na wafanyakazi wa kiwandani haziko rafiki kwa watoa huduma kutokana na kukosa vitu muhimu kama vile madirisha, pamoja na udogo wa ofisi hizo.

### 5.1.7 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wa eneo lililojengwa kiwanda juu ya umuhimu wa kiwanda hicho . Kwa kufanya hivyo itasaidia kupatiwa ulinzi shirikishi kwani wananchi wakishajua umuhimu na faida za kiwanda hicho ndio watatambua kua ile ni mali ya kwao na inahitaji kupatiwa ulinzi shirikishi zidi ya waharibifu na wapinga maendeleo.

2. Kamati inaishauri Wizara kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa matokeo ya tafiti zilizokwishafanyika juu ya aina gani ya mwani ambao una soko kubwa na una stawi vizuri ndani ya mazingira yetu ili kiwanda chetu kiweze kupata uhakika wa malighafi kutoka ndani ya nchi.

3. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara pamoja na Mkurugenzi wa Viwanda kwa kufanikiwa kufikia lengo la Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar kwa kusimamia ujenzi wa kiwanda hicho na pia kuhakikisha kuwa kinasimama kwani kufanikiwa kwa uwekezaji huu kutafungua fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu.

4.Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda washirikiane na Wizara ya Uchumi wa Buluu katika kuwasaidia wakulima wa mwani wapate vifaa vya kulimia pamoja na kuwezeshwa kwa mikopo ili wakulima hao waweze kuhamasika na kupata uwezo wa kuzalisha mwani kwa wingi.

5. Kamati inashauri Wizara kwa upande wa ajira hasa zile za kawaida ambazo hazihitaji utaalamu wa hali ya juu zitolewe kwa wananchi ambao wanaoishi maeneo ya karibu na kiwanda hicho ili waweze kunufaika juu ya uwepo wa kiwanda hicho.

6. Wafanyakazi wa kiwanda hicho wajengewe mazingira ya kupatiwa elimu (refresher courses) kila baada ya muda ili waweze kufanya kazi kwa kwa ufanisi wa hali ya juu na kupelekea kudumu kwa mashine zetu na vifaa vinavyopatikana kiwandani hapo.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ina dhamana ya kusimamia Sekta Kuu mbili ambazo ni Utalii na Mambo ya Kale. Sekta hizi hujumuisha Kamisheni moja, Idara nne, Mamlaka moja na Ofisi Kuu Pemba ambazo ni: -

1. Kamisheni ya Utalii Zanzibar
2. Idara ya Utalii
3. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
4. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe
5. Idara ya Uendeshaji  na Utumishi
6. Idara ya Mipango, Serana Utafitina
7. Ofisi Kuu Pemba

## 6.1 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa "Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria". Kwa sasa Wizara ipo katika hatua za utekelezaji wa mradi huo ambao ulianzwa kutekelezwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023. Katika mradi huu, maeneo yanayofanyiwa matengenezo ni pamoja na eneo la kihistoria la Mangapwani Unguja na eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu Pemba, eneo la kihistoria la Maruhubi na kuimarisha Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni – Unguja.

### 6.2 MRADI WA KUIMARISHA ENEO LA KIHISTORIA LA RAS MKUMBUU PEMBA.

Mradi huu unatekelezwa na kampuni ya **Yassin & Sons Limited**. Mradi huu umepangiwa **Tsh 2,407,316,675.00/=**. Katika kipindi cha robo mbili Julai – Disemba 2023/2024 mradi huu umepangiwa **Tsh. 1,750,000,000.00/=** na hadi sasa Mkandarasi ameshalipwa malipoyaawalijumlaya**Tsh.240,731,667/=**sawanaasilimia**13.76** na unatarajiwa kuchukua muda wa mwaka mmoja. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia **41**. Kazi zilizomalizika ni pamoja na kujengwa kwa jengo la kutolea huduma ambapo kwa sasa lipo katika hatua ya kuezekwa pamoja na kujengwa kisima. Hatua zinazoendelea kwa sasa ni kujenga hodhi la kuwekea maji lenye ujazo wa lita 36,000, kujenga mnara wa kuwekea tenki lenye ujazo wa lita 5,000 pamoja na kuomba umeme ambao kutoka unapopatikana hadi kufikia eneo husika ni kilomita 1.1.

### 6.3 CHANGAMOTO

1. Kuzorota kwa utekelezaji wa mradi huo kunakosababishwa na upatikanaji mdogo wa fedha kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipwa mkandarasi, hadi Kamati ilipotembelea katika eneo hilo tarehe 01/11/2023 imeelezwa kuwa mkandarasi amelipwa asilimia 10 tu sawa na Tzs 240, 731,667.5 na kubakiza Tzs 2,116,585,007.5 ambazo hazijalipwa kwa mkandarasi
2. Uwepo wa miundombinu ya barabara ambayo si rafiki kutoka mjini kuelekea Ras Mkumbuu, barabara hiyo inakwamisha jitihada za kumaliza mradi huo kwa wakati hasa kipindi cha mvua baadhi ya magari ambayo hutumika kubeba zana na malighafi mbalimbali za mradi kukwama njiani kutokana tope na uchakavu wa barabara hiyo.
3. Uingiaji wa wageni kiholela katika eneo hilo bila ridhaa au kibali maalum kutoka kwa Mamlaka husika hali ambayo huisababishia Serikali kukosa mapato yake.

### 6.4 MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inashauri Wizara kuhakikisha Mkandarasi anapatiwa fedha zake kwa wakati na kwa kiwango sahihi kilichopo ndani ya Mkataba ili aweze kutekeleza kazi zake kwa weledi mkubwa na kuweza kumaliza mradi huo kwa wakati uliopangwa ili kuepusha Serikali kuingia katika gharama kubwa katika kutekeleza mradi huo.

2. Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada ya haraka ya kuboresha miundo ya Barabara ya kuelekea Ras mkumbuu ili iweze kupitika kwa urahisi kwa wageni

wanaotembelea eneo hilo, aidha kusaidia kusafirisha kwa urahisi zana mbalimbali pamoja na malighafi ambazo zinatumika katika ujenzi wa Mradi wa Ras mkumbuu.

3. Kamati inaigiza Wizara ifanye utaratibu wa kudhibiti uingiaji holela wa wageni pamoja watalii mbalimbali wanaofika katika eneo hilo kwa kujisajili na kukusanya mapato kwa lengo la kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato Serikalini, aidha utaratibu huo utasaidia kulinda mali na zana za kihistoria zinazopatika katika mji uliozama ambapo baadhi ya wageni ambao hawajulikani hufanya utafiti katika maeneo hayo kwa kuzama chini ya bahari na kuchukua baadhi vitu vilivyomo ndani ya mji huo bila ya ruhusa ya Mamlaka husika.

### 6.5 MRADI WA KUIMARISHA ENEO LA KIHISTORIA LA MANGAPWANI UNGUJA.

Mradi wa Kuimarisha eneo la kihistoria la Mangapwani Unguja unatekelezwa na Kampuni ya Al - Hilal General Trading Limited. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 65. Mradi huu kwa sasa upo katika hatua za kuweka nguzo za uzio na geti na ukuta. Mradi huu utagharimuTsh 2,238,544,230/=na hadi sasa Mkandarasi ameshalipwa malipo ya kwanza ambayo ni jumla ya Tsh.368,223,755/=Sawa na asilimia 16.45 ya malipo yote.

Pia, mradi wa kuimarisha eneo la kihistoria la Maruhubi na Mahamamu ya Kidichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni – Unguja kwa sasa ipo katika hatua za manunuzi.

Aidha, Wizara inatekeleza mradi wa Utafiti wa kuangalia uwezo wa Zanzibar kuhimili wageni (Zanzibar Tourism Carrying Capacity) na utafiti unatekelezwa na kampuni ya AFRICOM na mshauri elekezi Profesa Haji Hatib Semboja ambapo kwa sasa mshauri elekezi ameshawasilisha Wizarani ripoti ya awali (Inception Report) ya Utafiti huo. Utafiti huo umepangiwa kutumia Tsh. 876,084,476.00 na hadi sasa wameshalipwa Tsh. 291,017,035 sawa na asilimia 33.21. Utafiti huu utasaidia Wizara kutathmini idadi kubwa zaidi ya watalii, eneo au vivutio vinaweza kumudu bila kusababisha uharibifu wa mazingira, vurugu za kijamii au kupungua kwa ubora wahuduma kwa wageni. Aidha, utafiti huu utasaidia kuhifadhi rasilimali za asili na kukuza usimamizi mzuri wa utalii endelevu.

## 6.6 CHANGAMOTO

1. Ukosefu wa ofisi kwa watendaji katika eneo la mradi , hivyo maafisa hulazimika kukaa katika sehemu zisizo rasmi.
2. Uhaba wa vitendea kazi kama vile gari za ufuatiliaji katika shughuli za miradi.
3. Kutopatikana kwa fedha za OC kwa wakati na inayopatikana ni ndogo ukilinganisha na mahitaji. Hali hii inapelekea kuzorota kwa miradi.
4. Ukiukwaji wa masharti ya vibali wakati wa kufanya ukarabati. Mamlaka kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ukarabati unafanyika kwa mujibu wa ramani na vibali vinavyotolewa.

## 6.7 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na umuhimu wa maeneo yetu ya kihistoria, Kamati inashauri Wizara ijipange vizuri katika kuhifadhi historia sahihi ya maeneo hayo ili kubakia uasili wake kwa vizazi vijavyo na kuwavutia wageni wanaotembelea maeneo hayo.

2. Kamati iinaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuipatia Wizara ya Utalii fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo kama zilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi ili kuweza kutekeleza majukumu yake ya msingi.

3. Kwa ajili ya utekelezaji bora wa malengo ya Wizara, Kamati inashauri Wizara ipatiwe vyombo vya usafiri (gari) kama ilivyowasilisha mahitaji yake.

## 6.8 KAMISHENI YA UTALII

Kamisheni ya Utalii Zanzibar inaongozwa kwa Sheria nambari 6 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake (Sheria nambari 7 ya mwaka 2012). Aidha, shughuli za utalii pia zinasimamiwa kwa Kanuni ya Utalii ya mwaka 2017, Sera ya Utalii ya Zanzibar ya mwaka 2018, Mpango wa Maendeleo Zanzibar (2021-2026), Dira ya Zanzibar 2050 na Mipango yote inalenga kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025.

Kimuundo, Kamisheni ina Idara tatu pamoja na ofisi ya Pemba. Majukumu ya Kamisheni ya Utalii yameainishwa katika Sheria ya Utalii nambari 6 ya mwaka 2009 kifungu nambari 4 (a- t).

Kamisheni ina mashirikiano makubwa na Bodi ya Utalii Tanzania ambayo ndiyo chombo kinachotoa miongozo kwenye sekta ya utalii nchini.

Kamati ilipata fursa ya kufanya ziara Tanzania bara kwa lengo la kujifunza na kujionea maeneo mbalimbali ya kihistoria ambayo yanavutia watalii na wageni mbalimbali kuja Tanzania kufanya utalii wa aina mbambali ukiwemo utalii wa kihistoria, michezo, na kujifunza tamaduni mbalimbali zilizomo ndani ya jamii ya Mtanzania hususan utamaduni wa mswahili.

Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo;

- Makumbusho ya hifadhi ya Taifa
- Kijiji cha utamaduni kilichopo mikocheni
- Bodi ya utalii Tanzania
- Kijiji cha Kaole kilichopo Bagamoyo

Kupitia ziara hiyo, Kamati imejifunza mambo mbalimbali kama ifuatavyo;

a) Mikakati mbalimbali inayofanywa na Bodi ya utalii ya kutangaza vivutio mbalimbali vya kitalii vilivyomo Tanzania kwa njia ya Kimtandao (Digital Platform) Kama vile Mlima Kilimanjaro, Hifadhi za Taifa kama vile Ngorongoro, Mikumi pamoja na vivutio vilivyopo visiwani Zanzibar kwa lengo la kuongeza idadi kubwa ya watalii kuja nchini mwetu.

b) Historia mbalimbali ikiwemo historia ya Binaadamu wa Kwanza kabla kuja kwa yesu kristo, mabaki ya vitu vya kale kama vile sarafu mbalimbali, zana za mawe, sahani za udongo n.k aidha kamati ilijionea kazi za Sanaa mbalimbali ikiwemo uchoraji, ufinyazi na tamaduni mbalimbali za mswahili.

c) Kamati imeendelea kujifunza makabila mbalimbali yaliyomo Tanzania pamoja tamaduni zake ikiwemo nyumba zao za asili, vyakula wanavyokula, mavazi, na ngoma zao za asili kupitia kijiji cha utamaduni kilichopo Mikocheni.

d) Kamati ilijionea mji wa Kihistoria wa Kaole uliopo Bagamoyo na kufanya ziara katika maeneo mbalimbali yakiwemo msikiti wa karne ya 13, kaburi la wapendanao, jengo la Ngome kongwe ya Bagamoyo, jengo la Ikulu ya Mjerumani pamoja na bandari ya Kwanza ya Bagamoyo.

## 6.9 CHANGAMOTO

1. Ukosefu wa ofisi kwa watendaji wa Kamisheni ya Utalii: Jengo linalotumika ni la kukodi na halina nasafi za kutosha kwa maafisa wote, hivyo maafisa hulazimika kukaa katika sehemu zisizo rasmi.

2. Idadi kubwa ya mapapasi kwenye sekta ya utalii inayopelekea usumbufu kwa watalii na upotevu wa mapato kwa Serikali.

3. Uhaba wa vyombo vya usafiri ambapo kamisheni ina majukumu ya kufanya kazi na polisi utalii ambao hawana usafiri wala kambi.

## 6.1.1 MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na uchakavu na udogo wa jengo la Kamisheni ya Utalii, Kamati inashauri Serikali kuipatia jengo la kisasa linalolingana na uzito wa kazi zake.

2. Kamati inaiomba Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kufanya shughuli za kitalii utakaowaruhusu vijana wetu kupata ajira kwa wingi bila ya kuathiri usalama wa wageni nakuongeza  pato la nchi yetu.

3. Kamati inashauri matumizi ya mifumo yazidi kuimarishwa ili kukusanya mapato mengi zaidi.

4. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati inaiagiza Serikali kuipatia Kamisheni ya Utalii usafiri wa kisasa kwa matumizi ya Polisi Utalii.

5. Kamati inaishauri Kamisheni ya Utatalii kufanya shughuli zake kwa kutegemea programu tofauti (program diversification) ili kuwavutia watalii zaidi na kuwa na uhakika wa mapato ya sekta ya utalii.

6. Kwa vile Kamisheni ya Utalii ni chombo kinachojitegemea kwa sasa, Kamati inaishauri Kamisheni itenge fedha zaidi kwa ajili ya kuutangaza utalii wa Zanzibar (tourism promotion) ili kupata watalii wengi zaidi.

7. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine kulitumia eneo la utamaduni wa Mzanzibari kwenye kijiji cha utalii Dar-es-salaam kwa kujenga nyumba na kuweka vielelezo vyote vya utamaduni wetu. Pia, Kamati inapendekeza kuanzishwa kwa kijiji cha utalii Zanzibar ili kulinda historia na utamaduni wetu kwa vizazi vijavyo.

### 6.1.2 HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo, maagizo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati una lenga kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele.

Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yote yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizo bora zaidi kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Kamati inatoa shukurani zake za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.